# Nipashe

Jumatano Februari 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580501

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Zanzibar** yatoa hadhari magonjwa ya kuambukiza

UKURASA 3



**Wanafunzi** 400 watumia chumba kimoja cha darasa

UKURASA 5

**Liverpool yajipanga kumsajili Ocampos**

UKURASA 21

# Dk. Mpango aanika alivyopigania uhai

• **Atoka** hospitalini baada ya siku 28, alilia viongozi waliofariki dunia... *Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (katikati), akilia baada ya kuwakumbuka baadhi ya viongozi waliofariki dunia hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika na kushoto ni Dk. Anthony Junda, wakijaribu kumtuliza, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuruhusiwa.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MWENYEKITI CCM AFARIKI DUNIA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Simiyu...

UKURASA WA 5

**PM ATAKA WATANZANIA KUENDELEA KUSHIKAMANA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania waendelee...


## BoT yapiga marufuku ada, kodi usajili wa Saccos, Vicoba

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Tatizo la vitambulisho NIDA lapata ufumbuzi

UKURASA 2


MICHEZO YANGA YAIANDALIA 'MAUAJI' KENGOLD UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# HABARI KITAIFA



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kulia), akiangalia kitambulisho kilichokamilika, baada ya kuhakikiwa katika kitengo cha kuhakiki ubora wa kadi zilizozalishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mjini Kibaha, mkoani Pwani, jana. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Dk. Arnold Kihaule. **PICHA: WMNN**

## Tatizo la vitambulisho NIDA lapata ufumbuzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameiagiza Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kukamilisha utoaji wa vitambulisho milioni 12 hadi ifikapo Julai, mwaka huu.

Simbachawene aliagiza jana baada ya kufanya ziara ya siku moja katika mamlaka hiyo mjini hapa kuona mitambo mipya inavyofanya kazi na kuondoa vikwazo vilivyokuwapo awali vya kuchelewesha utoaji wa vitambulisho.

Alisema awali NIDA ililenga kukamilisha kutoa vitambulisho milioni 12 Agosti, mwaka huu, lakini ametaka ihakikishe ifikapo Julai, mwaka huu, vitambulisho ambavyo wananchi wana namba zao, wavipate.

Simbachawene alisema mitambo ya zamani haikuwa na uwezo wa kutoa vitambulisho vinavyotakiwa na kwamba kwa sasa baada ya kufunga mitambo mipya, uzalishaji ni kadi 1,000 hadi 2,000 kwa saa na kwa saa 16 ni kadi 32,000.

Alisema baada ya kumaliza kadi 5,000,000 za zamani wataanza awamu ya pili ambayo uzalishaji utakuwa kadi 4,000 hadi 4,500 kwa saa na katika saa 16 zitazalishwa kadi 72,000 hadi 75,000.

Waziri alisema kwa sasa hakutakiwa tena na kikwazo cha kuchelewa kwa vitambulisho kutokana na kufungwa mitambo mipya.

Pia alisema wizara kwa sasa inaangalia uwezekano wa kukifanya kitambulisho cha taifa kutumika na taasisi zingine zikiwamo benki kumwondolea mwananchi kuzunguka na vitambulisho vingi.

## Mwenyekiti CCM afariki dunia

**Na Happy Severine,** MASWA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Simiyu, Enock Yakobo, amefariki dunia akiwa nyumbani kwake wilayani Meatu.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Simiyu, Mayunga George, ilisema kabla ya umauti, Yakobo aliugua malaria na kulazwa kwa wiki moja katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa.

Alisema Yakobo baada ya kupatiwa matibabu, aliruhusiwa kwenda nyumbani ambako alikuwa akiendelea kutumia dawa alizokuwa amepatiwa.

George alisema kifo cha mwenyekiti huyo ni pigo kwa wanachama wa chama hicho na wananchi wa mkoa huo. Alisema enzi ya uhai wake, Yakobo alikuwa mstari wa mbele kukipigania chama na kuyaunganisha makundi mbalimbali ndani na nje ya chama.

"Kama ambavyo mnamjua mwenyekiti, nashindwa hata kueleza sifa na jitihada alizokuwa akizifanya ndani na nje ya chama. Amekuwa na mchango mkubwa kwetu sisi na amesaidia kuondoa makundi ndani ya chama," alisema George.

Aliongeza kuwa enzi za uhai wake, mwenyekiti huyo alitumia muda mwingi kukitumikia chama na alikijenga na kuweka misingi mizuri kwa viongozi na wanachama kwa kufanya kazi kwa ushirikiano na upendo.

Alisema kwa sasa wanawasiliana na familia ili kujua taratibu za maziko na kwamba ratiba kamili itatolewa baadaye.


**NAMPULA AUCTION MART AND COMPANY LTD**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **NCBA BANK TANZANIA LIMITED** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa ambao wameshidwa kulipa deni wanalodaiwa na benki hiyo.
Mnada utafanyika mahari nyumba zilipo

| Jina la mdaiwa | Dhamana | Maelezo ya dhamana | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|
| Geoffoson INVESTMENT LTD | nyumba | Plot no 434 block "b" ct no 86418 kinyerezi wilaya ya ilala I.NO Geoffoson | 20/3/2020 |
| Geoffoson INVESTMENT LTD | nyumba | Plot no 616 block"s" ct no 36359 mbulu area, kahama I.NO | 17/03/2021 |
| LUSEKELO JOSEPH KASSANGA | nyumba | Plot no 1block"f" ct no 125899 malamba mawili wilaya ya ubungo I.NO LUSEKELO JOSEPH | 20/03/2021 |
| RAMADHANI NASOR MAULID | nyumba | Plot no 1029 ct no 104000 wilaya ya temeke | 22/03/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**
(a ) Mnunuzi atalazimika kulipa 25%ya bei liyofiki wakati wa mnada papohapo asilimia iliyobakia .75% italipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.
(b) Endapo mnunuzi atashidwa kulipaa silimia 25% siku ya mnada basi mshindiwa pili anahaki ya kuweka hela siku hiyohiyo .
(c) Mnunuzi akishidwa kutimiza sharti la 75% malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa
(d) Gharama za kubadilisha umiliki, kumtoa mtu kwenye nyumba na gharama nyingine zozote zitakazojitokeza itakuwa juu ya mnunuzi. .gharama zozote zitakazojitokeza nje ya utaratibu wa kibenki hatutahusikanazo

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA DALALI WA BENKI MOBILE: 0782757829, / 0719441711**


## Mpango aanika alivyopigania uhai

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameruhusiwa kutoka katika Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), alikokuwa akitibiwa na kueleza alivyoishi kwa mtungi wa oksijeni kwa takribani siku 28.

Dk. Mpango alisema hayo, jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuruhusiwa kutoka katika hospitali hiyo alipolazwa kwa siku 14.

"Leo ni siku 14 nimekaa hapa hospitalini nikihudumiwa hapa kwa siku 14. Nilikuja hapa na mtungi wa oksijeni. Leo ni siku ya tatu sijagusa kabisa mtungi wa aksijeni," alisema.

Alisema hivi sasa hali yake imeimarika vizuri kabisa ndiyo maana jopo la madaktari wameona anaweza kuruhusiwa na kuendelea na shughuli za kulijenga taifa.

"Sasa niko vizuri kabisa hata baadhi ya kazi nimeanza kuzifanyia hapa. Kwa wale rafiki zangu wanaotumia benki ya NMB, leo (jana) nina uhakika wameshaona kitu kimeingia tayari," alisema.

Pia alisema kuwa shukrani ya kwanza anaitoa kwa Mwenyezi Mungu kwa kumtendea makubwa, kutoka alipokuwa nyumbani kwa siku 14 akitibiwa na madaktari na hadi walipomhamishia hospitalini hapo kwa siku zingine 14.

"La pili kwa nafasi ya pekee sana, napenda kumshukuru Rais wangu, Dk. John Magufuli na familia yake. Nitasema tu ukweli hakuna siku ambayo hakuacha kunipigia simu na amekuwa akituma wasaidizi wake na madaktari wake kunihudumia. Sina maneno ya kumshukuru," alisema.

Aliwashukuru pia Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, Spika Job Ndugai na Watanzania wote kwa kufuatilia afya yake kila siku.

Katika hatua nyingine Dk. Mpango alijikuta akitoa machozi alipokumbuka vifo vya baadhi ya viongozi wa kitaifa na ndugu zake waliopoteza maisha hivi karibuni.

Aliwataja viongozi hao kuwa ni aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalimu Seif Hamad; Katibu Mkuu wa Kiongozi, Balozi John Kijazi na mwalimu wake, Prof. Benno Ndulu, aliyewahi kuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Mkurungenzi Mtendaji wa BMH, Dk. Alphonce Chandika, alisema huduma zinazotolewa hapo ni bora, hivyo akawasihi viongozi na Watanzania kwa ujumla waitumie kupata huduma za afya.

Dk. Chandika alisema watumishi wanafanya kazi kwa ari na ushirikiano na wataalamu wana vifaa vya kutosheleza kuwahudumia wananchi wote.

Pia alisema huduma zote zimeboreshwa na Dk. Mpango ametibiwa na madaktari wote wazalendo.

## HABARI KITAIFA

# BoT yapiga marufuku kodi, ada VICOBA

**Na Salome Kitomari,** MTWARA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema hakuna tozo au ada yoyote inayotakiwa kutozwa na mamlaka yoyote ya serikali kwenye usajili wa vikundi vidogo vya fedha hususan VICOBA.

Aidha, vikundi ambavyo vimetozwa fedha au vitatozwa fedha za usajili na halmashauri au manispaa yoyote vinatakiwa kutoa taarifa BoT ili hatua zichukuliwe.

Pia vikundi vimetakiwa kutokuwa chini ya mdhamini au Chama cha Akiba na Mikopo (SACCOS), bali vitatakiwa kusajiliwa moja kwa moja na halmashauri au manispaa pekee na kupewa cheti cha usajili ambacho kinatolewa bure.

Ufafanuzi huo ulitolewa jana na Meneja wa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilisha Fedha, Victor Tarimu (pichani), wakati akiwasilisha mada ya usimamizi wa watoaji huduma ndogo za fedha mjini Mtwara kwa waandishi wa habari wanaohudhuria mafunzo ya kuandika habari za uchumi, biashara na fedha.



Alitoa ufafanuzi kutokana na maswali ya waandishi wa habari juu ya uwezo wa taarifa za kutozwa kodi kwenye fedha za wanachama kila mwezi na mwisho wa mwaka.

"Hakuna fedha yoyote itayotozwa kodi kwenye mtaji ya wakopaji wala faida waliyoyapata wanakikundi mwisho wa mwaka," alifafanua.

Alisema usajili wa VICOBA bado haujaanza kwa kuwa walisubiri mwongozo wa mfumo wa kujaza taarifa za kikundi na kwamba vimekamilika ikiwamo kutoa elimu kwa maofisa maendeleo ya jamii ambao wanawajibu wa kutangaza katika maeneo yao usajili unaanza lini.

"Kumekuwa na maneno mengi ila taarifa rasmi ya BoT ni kuwa hakuna kikundi kinalazimika kuwa chini ya SACCOS au mdhamini. Kinachotakiwa wasajiliwe na wafuate matakwa ya kisheria," alisema Tarimu.

"Halmashauri au Manispaa hairuhusiwi kutoza fedha yoyote kwa kikundi. Kuna taarifa tulipata kuwa kuna vikundi vilitozwa Sh. 30,000 ya usajili. Ikitokea wakituandikia tutafuatilia na fedha zao zitarudi. Usajili hadi kupata cheti ni bure na hairuhusiwi kutoza fedha yoyote.

"Bila mifumo ingekuwa shida maana maofisa maendeleo ya jamii hawakuwa na elimu, wakitoka kwenye mafunzo ndani ya mwezi mmoja hadi miwili wanatakiwa wawe wamesajili vikundi. Kinachotakiwa kwa vikundi ni idadi ya wanachama, viongozi, katiba na muhtasari wa wanachama kuanzisha kikundi," alisema na kuongeza:

"Usajili unachukua saa mbili na baada ya hapo ndani ya siku 14 kikundi kinatakiwa kiwe kimepata cheti cha usajii kilichosainiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri husika."

### MADARAJA NA WALIOSAJILIWA

Kwa mujibu wa meneja huyo, kuna madaraja manne yaliyotambuliwa kisheria na kila moja lina kanuni zake na mamlaka iliyokasimiwa kusimamia.

Alisema daraja la kwanza ni benki zinazotoa huduma ndogo za fedha ambazo zinasimamiwa na BoT.

Daraja la pili ni taasisi zinazotoa mikopo bila kupokea amana za umma ikijumuisha kampuni za kukopesha, watoa huduma ndogo kwa njia za kudijitali na watu binafsi wanaokopesha.

Aidha, alisema hadi sasa wamepokea maombi 663, leseni 293 zimeshatolewa na mengine yamekataliwa na baadhi yako katika hatua za usajili hadi Februari 2, mwaka huu. Alibainisha kuwa zaidi ya waombaji wa kampuni binafsi za ukopeshaji baada ya kupewa masharti hawakurudi na wengi hawakuwa wamesajiliwa Brela na BoT kupata leseni ya kazi husika.

Alisema daraja la tatu ni la vyama vya ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS) ambavyo usimamizi wake umekasimiwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), na hadi sasa kuna maombi 241 kati ya 1,000 zilizopo.

Meneja huyo alisema kuwa daraja la nne ni la vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii (VICOBA, VSLAs), ambayo usimamizi wake umekasimiwa kwa mamlaka za serikali za mitaa.

Alisema utaratibu huu unakwenda kukabiliana na wagopaji sugu kwa kuwa taarifa za watu zitakuwapo kwenye mfumo ambao benki, taasisi za fedha, saccos na vikundi vitaona.

"Mfumo huo utaonyesha mwenendo wa mkopaji, kama amekopa sehemu A na anavyorejesha, lakini itaonyesha hata ankara mbalimbali anazolipa au halipi kama za maji, umeme, ni mfumo mzuri utasaidia sana kuepukana na mikopo chechefu," alisema.

### ADA KWA WATU BINAFSI/KAMPUNI

Kwa mujibu wa kanuni ya sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2017, watoa huduma ndogo za fedha wasiopokea amana ikiwamo kampuni za mikopo, watu binafsi wanaokopesha na wakopeshaji kwa njia ya kidijitali watatakiwa kulipa Sh. 500,000 kwa kampuni na Sh. 300,000 kwa watu binafsi.

# Zanzibar yatahadharisha magonjwa ya kuambukiza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imewataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya maradhi ya kuambukiza ikiwamo corona.

Tamko hilo lilitolewa jana na hayo yalielezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Dk. Khalid Salum Muhammed, na kusema hivi karibuni kumejitokeza wananchi wengi kusumbuliwa na maradhi ya homa ya mapafu, homa kali na shida ya kupumua.

Alisema serikali inaelewa jambo hilo na inalifuatilia kwa karibu sambamba na kuchukua jitihada kubwa kupitia wataalamu wa afya ili kudhibiti hali hiyo.

"Kama tunavyofahamu kuwa dunia imeendelea kuathiriwa milipuko mbalimbali ya maradhi, yakiwamo maradhi ya homa ya mapafu, homa kali, shida ya kupumua na maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19); hali hii inapelekea haja ya kuchukua tahadhari kwa ajili ya kulinda maisha ya wananchi wetu," alisema waziri huyo.

Alieleza kuwa wakati serikali inaendelea na jitihada hizo, ni vyema kuchukua tahadhari za kujilinda na maradhi hayo ili kupunguza maambukizi ya maradhi yanayoambukiza katika jamii.

Aidha, Dk. Khalid alisema kila mmoja anatakiwa kuzingatia kudumisha usafi wa mikono kwa kunawa mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au vitakasa mikono (sanitizers).

"Maeneo yote yanayotoa huduma kwa watu wengi ni vyema wahusika wakaweka sehemu na vifaa vya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni au vitakasa mikono," alisema Dk. Khalid na kuongeza:

"Tuepuke mikusanyiko isiyo ya lazima muda wote na pale tunapolazimika kukaa watu wengi kwa pamoja tukae kwa masafa ya angalau mita moja kati ya mtu na mtu."

Aliwataka wananchi kuvaa barakoa hasa zile zilizotengenezwa kwa vitambaa na barakoa hizo zifuliwe kwa maji na sabuni kabla ya kutumia tena.

Alisema kwa wale wenye dalili za kukohoa, mafua makali au shida ya kupumua wanatakiwa kuripoti katika kituo cha afya kilicho karibu ili kupata ushauri unaostahiki.


## NOTISI / TANGAZO

MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR (T) LTD, NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION (T) MART LTD, SUNDI AUCTION MART (T) LTD, SMARKCORE GROUP (T) LTD, WAUNGWANA AUCTION MART (T) LTD, BEST GROUP (T) LTD NA SALEI AUCTION MART (T) LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/No | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | ISSA SIXSTUSI SANGA | ISSA SIXSTUSI SANGA | GARI TOYOTA TOYOACE T173DNR | MBEYA | 10/03/2021 |
| ii. | KASSIMU MOHAMED MILALA | MOHAMED KASSIMU MILALA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MLAMLENI KATA YA TAMBANI - MKURANGA | 10/3/2021 |
| iii. | SAMWEL MAHANDO TEMBO | SAWEL MAHANDO TEMBO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | YANGEYANGE-WILAYA YA ILALA | 11/3/2021 |
| iv. | TAUSI SUBIRI KIBAIZI | MR&MRS TAUSI WINCHRAUS | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MSONGOLA-YANGE YANGE | 12/3/2021 |
| v. | LILIAN JOHN MUNUO | AGNESS PAULO MOKIWA | NYUMBA YENYE HATI | KIBAHA | 13/03/2021 |
| vi. | JONATHAN ZAWADI MHANDO | JONATHANI ZAWADI MUHANDO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MBEZI MSAKUZI | 14/03/2021 |
| vii. | VICTORIA PAUL BAMULANGE | VICTORIA PAUL BAMULANGE | GARI TOYOTA IST NO. T316 DMH | TABATA CHAMA | 10/3/2021 |
| viii. | WAMBURA RYOBA MASHANI | WAMBURA RYOBA MASHANI | NYUMBA | YANGEYANGE MSONGOLA-ILALA | 11/3/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

**Kwa mawasiliano zaidi; Tupigie simu no. 0713077474/0765999000.**

MAKALA MAALUM

# Madereva masafa marefu walivyowekewa mkakati kukabiliana na ugonjwa corona



Magari yakiwa katika msururu mpakani kusubiri madereva kupimwa Corona. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Na Romana Mallya**



Mmoja wa madereva akipimwa virusi vya corona.

TANGU kuibuka kwa virusi vinavyosababisha ugonjwa wa corona (COVID- 19), dunia imekuwa katika harakati za kupambana na tatizo hilo huku kila nchi, taasisi na watu vinafsi wakichukua hatua mbalimbali juu ya kijikinga.

Nchini Tanzania, kwa mfano, miongoni mwa hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa ni pamoja na kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kutumia vitakasa mikono (sanitizers), kuvaa barakoa na hata kutumia njia za asili kama vile kujifukiza, maarufu kama nyungu, na kula vyakula vya kinga kama vile malimau, tangawizi na vitunguu swaumu.

Kwa ngazi ya kijamii, watu wamekuwa wakishauriwa kukaa kwa nafasi kutoka mtu mmoja hadi mwingine hasa kwenye mikusanyiko kama vile ibada, mikutano na sehemu zenye makutano ya watu wengi. Taasisi mbalimbali pia zimekuwa zikitoa miongozi kwa wafanyakazi wao juu ya kijikinga na ugonjwa huo.

Moja ya taasisi hizo ni kampuni ya usafirishaji mafuta ya Primefuels Tanzania Limited ambayo imewaanzishia madereva wa masafa marefu utaratibu wa kusafiri na vifaa vya kujikinga na COVID-19 ili kuhakikisha wanakuwa salama wakati wote wawapo safarini.

Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu na Utawala wa Primefuels, Calvin Bhillon, alisema hayo hivi karibuni alipohojiwa na gazeti hili lilipotaka kujua kampuni inavyowalinda madereva wake na janga la corona hasa wanaovuka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Bhillon alisema baada ya mlipuko wa pili wa corona kutangazwa duniani, baada ya ule wa kwanza kutokea mwaka jana, wiki mbili zilizopita walirejea katika utaratibu wa mwaka jana wa kuwapatia madereva vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo, ili wavitumie pindi wawapo safarini.

"Kwa kuwa madereva wetu wanakwenda nchi mbalimbali, wiki mbili zilizopita tumeanza upya kuwapatia vifaa kama barakoa, vitakasa mikono ili wavitumie kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona," alisema.

Bhillon alisema kampuni yao ina madereva 367 ambao wamekuwa wakifanya safari katika nchi mbalimbali za Afrika zikiwamo Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Uganda, Malawi, Kenya, Rwanda na Zambia.

Utaratibu kama huo, alisema waliufanya mwaka jana wakati janga hilo la corona liliporipotiwa kwa mara ya kwanza mwezi Aprili. Kwa mujibu wa Bhillon, tangu kutangazwa kwa janga hilo la corona, kumekuwa na utaratibu wa madereva kupimwa afya kwenye mpaka wa nchi husika anapoingia na kueleza kuwa ziko baadhi ya nchi ambazo hazipimi.

"Kipindi cha nyuma ilikuwa unapimwa mfano Dar es Salaam unakwenda na majibu ya vipimo, lakini baadaye walikuwa wanahitaji kufanya vipimo tena lakini kwa sasa wanapimwa wakiwa wanaingia kwenye nchi husika," alisema.

Kuhusu gharama za vipimo vya corona, anasema kila nchi ambazo hutoa huduma hizo ina zake lakini wakilinganisha na kwingine Tanzania zipo juu.

Anaeleza kuwa kwa sababu utaratibu wa kuondoka na vyeti vya majibu ya corona kutoka Tanzania hauko tena, usumbufu ulioko ni ule wa dereva kusubiri majibu kwa siku mbili mipakani.

"Tangu mwaka huu uanze hatujapata kesi za madereva wetu kupimwa na kukutwa na corona, lakini kama kampuni tumeona ni vizuri wafanyakazi wachukue tahadhari," alisema.

Bhillon alibainisha kuwa utaratibu wa kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa sabuni maji tiririka kila wakati pamoja na matumizi ya vitakasa mikono na kuzingatia umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu, uliwasaidia madereva mwaka jana na ulipunguza maambukizi miongoni mwao.

Alisema kampuni yao ilikuwa ikihakikisha kila dereva alipokuwa safarini lazima awe na vifaa kinga ndiyo maana baada ya mlipuko wa pili kutangazwa, wameamua kurejea upya utaratibu huo. Bhillon alisema wito wao kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki ambazo wanakwenda ni kwamba waondokane na dhana kuwa Tanzania kuna corona, watu hawapimwi na majibu yanayotolewa ni ya uongo.

"Serikali ya Tanzania kupitia balozi zake wafikishe ajenda hii kwenye nchi za majirani zetu, ili kuhakikisha unyanyapaa kwa Watanzania wanaokwenda kwenye nchi hizo haupo tena mwaka huu kama ilivyojitokeza mwaka jana.

"Kulikuwa na unyanyapaa hasa kwa madereva wetu na usumbufu wa askari wakati mwingine wamekuwa wakiwakataza hata kushuka kwenye magari kupata huduma yalijitokeza kipindi cha nyuma," alibainisha.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania, Chuki Shabani, naye alishauri majibu ya corona kutoka nchi moja yaheshimiwe na nchi nyingine ili kuondoa usumbufu kwa madereva wanaosafirisha bidhaa mbalimbali.

"Wito wetu kama vile ifanyikavyo mpaka wa Tanzania na Kenya, wakipimwa waondoke na majibu na yaheshimike na kama kuna kupimwa nchi nyingine kusiwe na gharama yoyote," alisema.

Kiongozi huyo alisema mwanzoni mwa mwezi huu, lilitokea tukio la madereva wao watatu kufungiwa kwenye kontena baada ya kufika mpaka wa Burundi kwa madai kuwa wana virusi vya corona na baadaye walipelekwa hospitalini.

"Tulipokea malalamiko haya kwa madereva wetu wakitueleza kuwa walipofika mpakani walipimwa na wakaambiwa kwamba wana corona sasa walitupigia wakawa wanalalamika kuwa wameonewa kwa sababu wakati wote wa safari walikuwa na utingo wao wakiwa wanakula na kulala pamoja kwenye gari na kuhoji mbona wao ni wazima lakini madereva tu ndio waonekane na corona," walilalamika.

Shabani anasema baada ya vipimo hivyo madereva hao wakiwa na wenzao wanane kutoka nchi nyingine walichukuliwa na kufungiwa kwenye kontena na baadaye walipelekwa hospitalini na mpaka hivi karibuni walikuwa wametoka.

**UTARATIBU WA AWALI**

Baada ya janga la corona kuripotiwa kwa mara ya kwanza mwaka jana, moja ya makundi ambayo yalitakiwa kuchukua tahadhari ni pamoja na madereva wa malori.

Mei mwaka jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (wakati huo), Ummy Mwalimu, alipokutana na madereva, aliwaambia wahakikishe wanakula vyakula ambavyo vitalinda kinga zao za mwili na wasiache kupiga nyungu.

Waziri Ummy alizungumza na kundi hilo mwezi huo wakati upimaji wa madereva wa kampuni za malori zinazosafirisha mizigo nje ya nchi ukifanyika katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko Mabibo, Dar es Salam.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Maabara hiyo, Ambele Mwafulango, katika takwimu zake alizozitoa alisema kwa siku walikuwa wakiwapima madereva 200 walioko jijini Dar es Salaam na kwa wale walioko mikoani waliweka utaratibu maalum wa kuchukuliwa sampuli ambazo zilikuwa zinatumwa kwa ajili ya vipimo.

"Katika maabara hii ya Mabibo tuna mashine mpya tano ambazo ndani ya saa 24 zinapima vipimo 1,800, hii imetufanya kupima vipimo vingi zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa katika maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko ofisi za NIMR (Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu) jijini Dar es Salaam. Tulikuwa na mashine mbili ambazo zilikuwa zinapima vipimo 300 hadi 400 jambo ambalo lilikuwa linachelewesha utendaji wetu wa kazi," alisema.

Serikali iliweka utaratibu maalum kwa ajili ya madereva wa malori wanaosafirisha mizigo nje ya nchi kwa kufanyiwa vipimo vya corona kabla ya kusafiri ili kuhakikisha hawana maambukizi na kuwaepusha na usumbufu wawapo safarini.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 400 wakaa darasa moja chini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI 400 wa Shule ya Msingi Kabale katika Halmashauri ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, wanakaa chumba kimoja cha darasa huku wengine wakiwa wamekaa chini kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Shule hiyo ina wanafunzi 1,900 ikiwa na vyumba vya madarasa vinane, huku darasa moja likitumiwa kama ofisi ya walimu.

Aidha, wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili wanalazimika kusoma kwa awamu huku darasa la kwanza wakiingia asubuhi na darasa la pili wakiingia mchana.

Hayo yalibainishwa jana katika shule hiyo na Mwalimu wa Taaluma, Kurwa Lufungulo, wakati wa kukabidhiwa vifaa vya ujenzi vilivyotolewa na kampuni ya Ako Group vyenye thamani ya Sh. milioni tano.

"Tatizo hili limesababishwa na ongezeko la wanafunzi. Kila mwaka tuna vyumba vinane vya madarasa kimoja tunakitumia kama ofisi ya walimu na wanafunzi wanakaa watano katika dawati moja," alisema Lufungulo.

Naye mwanafunzi Perepetua Leonard, alisema wanakabiliwa na uhaba wa madawati na kwamba kwa sasa wanafunzi 1,900 wanakaa kwenye madawati 216, huku darasa la kwanza, pili na awali wakikaa chini wakati wa masomo.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Ntana Kilagwire, Meneja Mkuu wa Ako Group, Athanas Kahindi, alisema wametoa mifuko 45 ya saruji, nondo 35, mbao, mchanga malori 10 na mawe lori 10 na Sh. 600,000 ambazo zitatumika kulipa mafundi wakati wa ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Akipokea vifaa hivyo, Dk. Kilagwire alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kusema kwa sasa wameunda kamati ya ujenzi ambayo itasimamia ujenzi wa madarasa mapya na kuwaomba wazazi na wadau wengine wa elimu kuchangia ujenzi huo.

## Mgomo daladala na maduka waendelea

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, wameiomba serikali kuona umuhimu wa kufanya mazungumzo na wafanyabiashara, ili kumaliza mgomo uliosababisha kufungwa kwa maduka, masoko na mabasi ya abiria ulioingia siku ya pili jana.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti mjini Songea jana, baadhi ya wakazi hao walisema tatizo la wafanyabiashara kugoma limesababishwa na mabasi kuzuiwa kuingia mjini Songea na kulazimika kuishia kituo kikuu cha mabasi kilichoko Shule ya Tanga umbali wa kilomita 17. Dikson Ngonyani, mkazi wa Ruhuwiko Manispaa ya Songea, alisema njia sahihi ya kutafuta maridhiano ya pamoja kati ya wadau wa maendeleo na serikali, ni lazima kukaa na kusikiliza malalamiko yaliyopo na siyo kutoa maagizo mazito ambayo hayawapi nafasi wananchi kusikilizwa.

Ngonyani alisema kutokana na mgomo huo, nauli ya kutoka Songea kwenda Namtumbo imepanda hadi Sh. 7,000 kutoka Sh. 2,500 na kutoka Songea kwenda Mbinga sasa ni Sh. 10,000 badala ya Sh. 4,000.

Alisema kuwa nauli ya kutoka Shule ya Tanga kwenda Songea Mjini kwa bodaboda ni kati ya Sh. 7,000 hadi 15,000 badala ya nauli ya zamani Sh. 5,000, jambo ambalo limeonekana kuwa ni kero kwa wananchi ambao wengi wao wana hali mbaya kiuchumi.

Salumu Brashi, mkazi wa Namtumbo, alisema uamuzi wa jana wa serikali kuwataka wafanyabiashara warudi kufungua biashara zao ndani ya saa 24 ni agizo zito ambalo bado linaleta shida kwa wakazi wa Songea kwa kuwa maduka bado yamefungwa.

Meya wa Halmashauri ya Manipsaa ya Songea, Maiko Mbano, alisema nia ya halmashauri ni kuwataka wafanyabiashara waendelee kufanya shughuli zao kama kawaida na siyo vinginevyo, lakini kwa wafanyabiashara ambao bado wanaendekeza huo mgomo, wanakwenda tofauti na maagizo ya serikali.



Makamu Mwenyekiti wa Kampuni ya Gem Tanzanite, Osman AbdulSattar (kushoto), akiwahudumia baadhi ya watu waliotembelea banda lake, kwenye maonyesho ya kitaifa ya uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania 2021, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## PM ataka Watanzania kuendelea kushikamana

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania waendelee kushikamana katika kipindi hiki ambacho dunia ina mahangaiko makubwa na magonjwa mbalimbali ya maambukizi.

"Tuendelee kumtegemea Mwenyezi Mungu kama Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli alivyotusisitiza na tuendelee kuiamini serikali na jitihada za viongozi wake tutapata utulivu."

Waziri Mkuu aliyasema hayo, juzi, aliposhiriki mazishi ya mfanyabiashara maarufu katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Ally Nalaga, yaliyofanyika Mnazimmoja Lindi. Alisema magonjwa hayo yameleta tafsiri tofauti na wakati mwingine kutokuwa na utulivu, kwani watu wanatishana sana, hali ambayo inawafanya wasiwe na amani na kuwajengea hofu.

Waziri Mkuu alisema serikali inaendelea kufuatilia mwenendo wa aina zote za magonjwa ambayo yanawakabili wananchi katika maeneo mbalimbali nchini na kuyatafutia tiba.

Hata hivyo, Waziri Mkuu aliwasisitiza wananchi waendelee kuchukua tahadhari ya kila ugonjwa. "Ukisikia Ukimwi kuna tahadhari zake, ukisikia kipindupindu kina tahadhari zake."

Pia Waziri Mkuu aliwaomba viongozi wa dini zote nchini waendelee kuliombea Taifa na viongozi ili liendelee kuwa na amani na kimbilio kwa walipoteza amani.

Akimzungumzia marehemu Nalaga, Waziri Mkuu alisema alikuwa mcheshi na mwenye upendo kwa kila mtu na alijitoa sana katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii.


NAMPULA AUCTION MART AND COMPANY LTD

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **NBC BANK TANZANIA** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa wao ambao wameshidwa kulipa deni wanalodaiwa na banki hiyo.
Mnada utafanyika mahari nyumba /dhamana zilipo

| Jina la mdaiwa | Jina la dhamana | dhamana | Maelezo ya dhamana | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|
| MMETA KAOMBWE SAIDI | MMETA KAOMBWE SAIDI | NYUMBA | Ct no 24918 LR MWANZA ,LO NO370508,PLOT NO896"R"CHEMCHEM MANISPAA YA TABORA I.N.O.MMETA SAID KAOMBWE | 13/3/2021 |
| KITWAN MIRAMBO | KITWAN KASONGO MIRAMBO | nyumba | Ct no 47080LR MWANZA L.O.NO 479617 PLOT NO 85 BLOCK "E" BARABARA YA MWANZA ROAD MANISPAA YA TABORA | 14/3/2021 |
| MASUDI OMARI OTHMANI | MASUDI OMARI OTHMANI | NYUMBA | CT NO 22035 LR MWANZA L.O.NO 229290 PLOT NO 19 BLOCK"EE" MABATINI MANISPAA YA TABORA INO MASUDI OMARI OTHUMANI | 14/3/2021 |
| MASUDI OMARI OMARI | MASUDI OMARY ATHUMAN | NYUMBA | PLOT NO 19 BLOCK"EE" MABATINI MANISPAA YA TABORA VALUED BY MAJENGO ESTATE DEVELOPERS LTD | 14/3/2021 |
| JEREMIAH .F MANYIWA | IDDY RAMADHANI SHABAN | NYUMBA | CT NO 40920,-LR MWANZA L.O.NO 479552 POLT NO 439 BLOCK "L" KANYENYE, MANISPAA YA TABORA | 13/3/2021 |
| JOHN .N. MAGINA | JOHN .N. MAGINA | NYUMBA | I.N.O IDDY RAMADHANI SHABAN CT NO 21505 LO,NO 181753,PLOT NO 827 BLOCK "Q"(HD) NYASUBI, KAHAMA I.N.O JOHN NDALAHWA MAGINA | 17/03/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

(a ) Mnunuzi atalazimika kulipa 25%ya bei liyofiki wakati WA mnada papohapo asilimia iliyo bakia .75% italipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.
(b) Endapo mnunuzi atashidwa kulipaa silimia 25% siku ya mnada basi mshindiwa pili anahaki ya kuweka hela siku hiyohiyo .
(c) Mnunuzi akishidwa kutimiza sharti la 75% malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa
(d) Gharama za kubadilisha umiliki, kumtoa mtu kwenye nyumba na gharama nyingine zozote zitakazojitokeza itakuwa juu ya mnunuzi. .gharama zozote zitakazojitokeza nje ya utaratibu wa kibenki hatutahusikanazo

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA DALALI WA BENKI MOBILE: 0782757829, / 0719441711

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ya kujilinda ni muhimu nyakati hizi

**VIONGOZI** mbalimbali wa serikali wamesisitiza wananchi kuchukua tahadhari, ikiwamo kukaa umbali wa mita moja, kuepuka misongamano na safari zisizo za lazima, kuvaa barakoa na kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni pamoja vitakasa mikono.

Aidha, viongozi wakuu wa serikali wamesema hakuna marufuku yoyote ya kuvaa barakoa, lakini msisitizo mkubwa ni tahadhari na kumwomba Mungu kwa bidii na ndiyo maana Rais John Magufuli alitangaza maombi ya siku tatu kwa waumini wa dini zote.

Tahadhari hizi zimesisitizwa pia ulimwenguni na kuna nchi nyingi zimefungia wananchi wake kutokana na kasi ya maambukizi ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona.

Kama ambavyo msisitizo wa sasa wa serikali ni kuwa Tanzania siyo kisiwa kutokana na kupakana na nchi mbalimbali ambazo zote na zimekumbwa na maambukizi.

Maana yake hata nchini tunaweza kupata maambukizi, hivyo ni muhimu kuchukua tahadhari ya kujikinga kwa nguvu zote kuhakikisha tunakuwa salama muda wote.

Lakini bado tunaendelea kupokea wageni na watalii wanaokuja kwa sababu tofauti tofauti, ambao wanaingia kwa njia nyingi. Hata hivyo, kwa jinsi virusi vya corona vilivyo, mtu anaweza kupata wakati wowote na mahali popote.

Msisitizo ni muhimu, laini bado tunaona kuna jitihada za makusudi zinatakiwa kufanyika kuhakikisha tahadhari inachukuliwa katika vyombo vya usafiri wa umma kama mabasi, daladala na mwendokasi, ambako maisha yaendelea kama kawaida licha ya kuwapo changamoto ya upumuaji.

Kadhalika, katika maeneo ya biashara ule utaratibu wa kuhakikisha kila eneo kuna maji tiririka na sabuni na mtu anawe kabla ya kuingia kununua au kupata huduma yoyote ni muhimu sana.

Pia, katika maeneo ya taasisi za elimu na shule ambazo mwaka jana zilikuwa na mwongozo wa kuchukua tahadhari, tunaona ni muhimu kwa sasa wakatekeleza ili kuendelea kubaki salama.

Tunasema tahadhari ni muhimu sana ili kuendelea kujilinda na corona inayosumbua dunia kwa sasa. Mathalani unapotembelea kituo kikuu cha mabasi Ubungo ambacho kinatumiwa na watu wa mataifa mbalimbali, jambo la kusikitisha hakuna tahadhari yoyote.

Pia, bado hakuna msisitizo katika kuvaa barakoa kwa wasafiri na watoa huduma, jambo ambalo tunaona ni muhimu sana likafanyika kwa kuwa Ubungo ni kituo kinahudumia watu wengi.


Pia ni muhimu viongozi wa serikali za mitaa, vitongoji na ngazi nyinginezo kushirikiana na wataalamu wa afya wakatoa elimu ya uvaaji wa barakoa, ambao wakati mwingine bila kufuata masharti ni rahisi kusambaza virusi.

Tunaamini wananchi wakielimishwa watafuata na kuchukua hatua madhubuti, kama ilivyofanyika kwenye maradhi mengine ambayo yamewahi kuisumbua dunia na nchi kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Zisikike sauti kudai nafasi kwa wanawake

Na Mwandishi Wetu

**UPO** msemo kuwa uchaguzi mmoja ukiisha huanzisha mwingine. Kwa hiyo baada ya kumalizika uchaguzi wa Oktoba 2020 yanayofuata sasa ni maandalizi ya uchaguzi wa 2025.

Hoja yangu ni kutaka mikakati iwape nafasi wanawake kwa vile baada ya uchaguzi mkuu sauti za uteuzi wa wanawake kushika nyadhifa mbalimbali zimeanza kupoa moto.

Itakumbukwa mwaka jana ulikuwa msimu wa masuala ya wanawake kuzungumzwa kila upande na zilisikika sauti kuhimiza uteuzi wao kuwa wagombea kwenye majimbo au kata wakati wa uchaguzi mkuu.

Ilikuwa habari kubwa ya vyama kwa sababu ilionekana kuwa kuteuliwa kinamama kushika nyadhifa hizo majimboni au kwenye kata kilikuwa kigugumizi kinachovipata vyama vingi. Vyama vinaoongozwa na hofu kuwa iwapo watapelekwa majimboni au kwenye kata hawatachaguliwa.

Vipo baadhi ya vyama viliwapa kinamama nafasi za kugombea ubunge, urais na hata udiwani na kimojawapo ni ADC.

Kiliteua kinamama kushika nafasi hizo kwenye majimbo yote ya Dar es Salaam na katika kata pia. Kampeni za kuhimiza uteuzi wa wanawake zilikuwa zinawahamasisha Watanzania kuwachagua wanawake kushika nafasi mbalimbali za kuongoza taifa kwani wana sifa zikiwamo umakini na utulivu, uadilifu na uchungu kwa watoto na familia zao.

Lakini kampeni kwa vyama zilivihimiza kubeba jukumu la kuwapa wanawake nafasi za uongozi wa kuchaguliwa kwa misingi ya kuheshimu ajenda na usawa wa kijinsia. Leo inafaa tena ajenda ya kuwatetea wanawake kupewa nafasi tena iwe endelevu hata baada ya miezi mitano ya uchaguzi.

Vyama vinatakiwa kuendelea kuweka mbele ajenda za kuwapa nafasi na kujadili mikakati ya kuwawezesha kinamama kushiriki kwenye uchaguzi bila vikwazo. Huu ndiyo wakati wa kuanza kuhamasisha tena vyama vya siasa pamoja na Watanzania kubadilisha mitazamo na kufuta mawazo hasi kwamba kinamama hawawezi. Wanawake wanafanya kazi kubwa na nzuri ndani ya serikali zote kuanzia awamu ya kwanza hadi ya tano.

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na sasa ni jambo ambalo linatosha kuamua kuwapa nafasi kwenye uchaguzi ujao wa 2025. Baada ya uchaguzi ndiyo wasaa wa vyama kutengeneza uhusiano mwema na wananchi ili uchaguzi ufanyike kwa misingi ya kijinsia, uhuru na wa haki tena unaokubalika.

Hivyo ni lazima vyama vitambue umuhimu wa kushirikisha wanawake na viwe na uelewa kwamba wanawake wamechoshwa na kauli kuwa ukishindwa kubali matokeo.

Kuwaandaa wanawake kuwa wagombea wa majimbo na kata nyingine za 2025 ni jambo linalotakiwa kuanza kuandaliwa sasa na hata kama watajitokeza wagombea wanaume mchujo ufanyike kwa haki.

Lakini, pamoja na kuwapa nafasi ni vyema vyama vianze kuwapa jukumu la kuviongoza.

Kina mama waanze kupewa majukumu ya kuongoza vyama na kufahamika kwa wananchi badala ya vyama vyote kuongozwa na wanaume ambao ndiyo wanaojitokeza na kupewa kipaumbele kwenye uchaguzi kwa kuwa wanafahamika.

Lakini, ili wanawake wapigiwe kura ni muda pia wa kufikiria namna bora ya kufanya siasa ili kila chama kinadi sera zake kwa wananchi na kuwatangaza wanawake badala ya kutegemea muda finyu wakati wa kampeni za uchaguzi. Ni wakati pia wa vyama visivyo na ruzuku kutafuta njia bora ya kuwaandaa wanawake na kuwafikisha kwa wapiga kura wanaowalenga.

Sababu za wanawake wengi kushindwa kushiriki kwenye kampeni za majimboni na kata ni pamoja na ukosefu wa pesa.

Katika mikakati ya kuandaa uchaguzi wa 2025 vyama vinatakiwa kuunga mkono wanawake kwa kuwa uchaguzi ni gharama na zinahitajika pesa nyingi kwenye kampeni.

Aidha, huu ndiyo muda wa kupata majibu ya maswali ya wapi pa kupata fedha hizo.

Mathalani, mkutano mmoja wa kampeni kwenye jimbo unaelezwa kuwa hugharamia takribani Sh. 1,000,000 nacho ni kiasi cha chini mno.

Vyama vianze kupanga mikakati ya kuwaandaa kinamama ili isiwe ni maneno zaidi kuliko vitendo.

# Jaji ataka mahakimu kuheshimu viapo

**Na Mwandishi Wetu,** LUSHOTO

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amewataka mahakimu wakazi wapya 71 kuamua mashauri kwa kuzingatia viapo vyao vinavyowataka kutenda haki pasipo kuangalia rangi, dini, chama, umri wala jinsia ya mtu.

Akifungua juzi mafunzo elekezi kwa mahakimu yanayofanyika katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama, mjini hapa, Jaji Kiongozi alisema uamuzi wa mashauri yatakayofanywa na mahakimu hao lazima yazingatie sheria, ushahidi uliopo na miongozo ya kimahakama na si vinginevyo.

"Msiamue mashauri hayo kwa chuki, huba, tetesi, hisia, kwa misukumo na mihemko. Nendeni mkawe mwarobaini wa kutoa suluhisho kwenye maeneo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wananchi katika mahakama za mwanzo," alisisitiza.

Jaji Feleshi aliyataja baadhi ya mashauri hayo kuwa ni ya mirathi, mgawanyo wa mali za ndoa, matunzo na hifadhi ya watoto pia kukazia na kutimiza hukumu.

Aliongeza kuwa wajibu wao ni kuwa makini na kuchukua tahadhari kwa kuwa uamuzi mbaya juu ya maeneo haya huumiza makundi maalumu yanayohusisha watoto, wajane, wagane na wazee, hivyo kuondoa imani ya wananchi kwa mahakama.

Pia Jaji Kiongozi aliwakumbusha maofisa hao wa mahakama kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuharibu taswira ya mahakama kama matumizi ya lugha chafu, kujigeuza miungu watu, mavazi yasiyozingatia maadili ya kazi, kujihusisha na mapenzi, ubabaishaji, ulevi na kuchelewa kuanza mahakama.

Sambamba na hayo aliwataka kuacha kuingilia au kuhoji maswali wakati kesi ikiendelea kwa kiwango cha kupitiliza, kuchelewesha uamuzi na kutotoa nakala za hukumu. Alisema mambo haya ni kinyume cha maadili ya utumishi wa mahakama.



Waziri wa Madini, Doto Biteko (kulia), akikabidhi moja ya tuzo ambayo Kampuni ya Barrick kupitia migodi ya North Mara, Buzwagi na Bulyanhulu ilishinda kwa Meneja Mkuu wa Migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu, Benedict Busunzu, wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliomalizika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka muda ulipaji kodi

**Na Veronica Kazimoto,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, ameipongeza Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kutoa elimu kwa mlipakodi, akiishauri kuongeza muda kwa kampeni hiyo kufanyika mlango kwa mlango.

Amesema wiki moja iliyopangwa kwa kampeni hiyo kufanyika mkoani hapa haitoshi kutokana na umuhimu wa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara.

Akizungumza jana na timu ya maofisa wa TRA wanaofanya kampeni hiyo mkoani hapa, Rubirya alisema kutembelea wafanyabiashara duka kwa duka siyo kazi rahisi, hivyo inahitaji muda wa kutosha ili kuhakikisha wafanyabiashara wote wanapata elimu hiyo muhimu.

"Ninawapongeza sana TRA kwa kuendesha utoaji wa elimu hii ya mlango kwa mlango katika mikoa mbalimbali na hatimaye mmefanikiwa kufika hapa Njombe.

"Lakini, huu muda wa wiki moja hautoshi, ninashauri siku nyingine mpange siku za kutosha ili kila mfanyabiashara anufaike na elimu hii," alisema Rubirya.

Mkuu wa mkoa huyo aliongeza kuwa elimu inayotolewa na TRA, itasaidia kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi kwa manufaa ya nchi na kuchochea maendeleo.

"Kama kuna eneo ambalo linasaidia katika ukusanyaji kodi, ni kuhakikisha wafanyabiashara wengi zaidi wanakuwa na elimu ya kodi ambayo itawasaidia kuongeza uelewa na hatimaye kujisikia fahari kwenda kulipa kodi," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara wa mkoani hapa baada ya kutembelewa na maofisa wa TRA, walisema utaratibu huo ni mzuri na utasaidia kuwapa elimu ya kutosha wafanyabiashara wengi na kuacha kuogopa maofisa wa TRA pindi wanapokuwa wanapita kwenye maeneo ya biashara zao.

Bahati Mtweve, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema: "Kwa utaratibu huu, ninadhani hakuna mfanyabiashara yeyote atakayekuwa anawaogopa TRA kwa kuwa wengi watakuwa na uelewa wa kutosha na watahamasika kulipa kodi kwa wakati."

Winfrida Mponela, mfanyabiashara mwingine mkoani hapa, alisema elimu inayotolewa na TRA katika kampeni hiyo, imewasaidia kufahamu zaidi juu ya utunzaji wa kumbukumbu.

Alisema kufika kwa maofisa wa TRA mkoani hapa, pia kumewawezesha wafanyabiashara kujua mambo mengi yanayohusu kodi.

"Kwetu sisi tumeona ni faida sana kutembelewa na maofisa wa TRA kwani wametupatia elimu ya matumizi sahihi ya mashine ya EFD kama sehemu ya utunzaji wa kumbukumbu na hii itatuepusha na faini zisizo za lazima ambazo mtu anapewa kwa kosa la kutokutoa risiti," alisema Mponela.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara mjini Njombe, Eliud Pangamawe, aliwaomba maofisa wa TRA, akiwamo Meneja wa Mkoa wa Njombe, Shabani Musibu, kuendelea kutoa elimu hiyo kila mara, ili kuondoa dhana iliyokuwa imejengeka awali kwamba TRA ni adui wa wafanyabiashara.

"Mnatakiwa kufanya kampeni hii mara kwa mara ili kuongeza ukaribu na urafiki kati yetu sisi na ninyi na pia kuondoa dhana potofu ya kusema ninyi ni maadui zetu," alisema.

Kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani Njombe imelenga kuwajengea uelewa wa kutosha wafanyabiashara na walipakodi kwa ujumla juu ya masuala mbalimbali yanayohusu kodi, kusikiliza maoni yao kwa ajili ya kuboresha huduma za TRA, kuwakumbusha kulipa kodi stahiki na kwa wakati, kusikiliza kero za kikodi walizonazo na kuzitafutia ufumbuzi.

# Kagera yakusanya kahawa ya bil.96/-

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKOA wa Kagera umekusanya kahawa ghafi ya kilo milioni 78.3 yenye thamani ya Sh. bilioni 96.4 kutoka kwa wakulima katika msimu wa mwaka 2020/21 unaoelekea kumalizika.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema jana kuwa kiwango hicho kimevunja rekodi ambayo haijatokea kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita.

Gaguti aliwapongeza wakulima wa zao hilo kwa kuzingatia maelekeo ya kitaalamu, yaliyowezesha makusanyo ya kahawa kuongezeka kutoka kilo milioni 52 za msimu wa mwaka 2019/20.

"Ukiangalia kumbukumbu msimu huu, makusanyo yamepanda zaidi maana hata msimu wa mwaka 2018/19 tulikusanya kahawa ghafi kilo milioni 58. Niombe tunapokaribia kuanza msimu mpya Mei, mwaka huu, wadau wote wa kahawa tulinde mafanikio tuliyoyapata," alisema.

Jenerali Gaguti alisema mafanikio hayo yanapaswa kulindwa kwa kuendelea kutumia mbinu na njia bora za kilimo, kuboresha mashamba na kuitunza kahawa kuanzia shambani mpaka sokoni ili iendelee kuwa na ubora unaokubalika kimataifa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**TANGAZO KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOs)**

Mashirika yote Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) yanakumbushwa kuwa yanatakiwa kuwasilisha taarifa zake za mwaka 2020 pamoja na kulipa ada ya mwaka husika (Annual Subscription Fee) ambayo ni; Shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) kwa Mashirika ya Kitanzania (Local NGOs) na Dola za Marekani Mia Moja (USD 100) kwa Mashirika ya Kimataifa (International NGOs).

Matakwa hayo ni kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya **56**, Kifungu cha **29(1)(a) &(b)** na marekebisho yake ya mwaka 2005 na 2019.

Mwisho wa kuwasilisha taarifa hizo ni tarehe **15 Aprili, 2021** Saa **9.30** Alasiri. Aidha, baada ya tarehe na muda uliopangwa kupita, malipo ya ada yatalipwa pamoja na faini kama ifuatavyo; Shilingi Laki Moja (100,000/=) kwa Mashirika ya Kitanzania (Local NGOs) na Dola za Marekani Mia Tatu (USD 300) kwa Mashirika ya Kimataifa (International NGOs).

Taarifa zote na malipo ni kupitia mfumo wa ***nis.jamii.go.tz*** kwa kufuata maelekezo (User Guide).

Limetolewa na;

Vickness G. Mayao
**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**
**Tel: 0737 569 583/ 0737 569 584**
**Website: www.jamii.go.tz/ www.tnnc.go.tz**

# Taasisi yajitosa kufadhili masomo udaktari, uhandisi

**Na Daniel Limbe,** KARAGWE

LICHA ya serikali kutumia fedha nyingi kugharamia mikopo ya elimu ya juu, baadhi ya taasisi za kiraia zimeonyesha nia ya kutoa ruzuku na ufadhili kwa vijana wa kike kusomea udaktari na uhandisi.

Moja ya taasisi hizo ni shirika lisilo la kiserikali la Mavuno lililoko wilayani Karagwe mkoani Kagera.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mavuno, Charles Bahati, alisema juzi kuwa ni matarajio yao kuwasaidia vijana wa kike kusoma fani za udaktari na uhandisi Ujerumani, Sweden na Marekani ili kuongeza wataalamu wa fani hizo.

"Mpango wetu unalenga kuongeza wataalamu wa fani hizo sambamba na kupunguza malalamiko ya vijana wengi wa elimu ya juu kukosa mikopo kutokana na uwezo wa serikali," alisema Bahati.


Alisema mpango huo unafanyika kwa ushirikiano wa karibu na marafiki wa shirika hilo kutoka katika nchi hizo.

"Ili kufikia malengo tuliyojiwekea, shirika letu limeanza ujenzi wa shule ya kidato cha tano na sita ya "Mavuno Girls Model" ili kutoa fursa kubwa kwa wanafunzi wa kike mkoani Kagera kunufaika na ruzuku na uhisani huo. Tutakuwa tumeipunguzia mzigo serikali na jamii kwa ujumla," alisema.

Mbali na kulipongeza Shirika la Mavuno, Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Geofrey Mheluka, alisema limekuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa wilaya za Karagwe na Kyerwa, hasa katika nyanja za kilimo, maji na nishaji ya umeme jua (solar).

Heluka alitumia fursa hiyo kuzitaka taasisi zingine za kiraia wilayani hapa kuiga mfano wa Mavuno kwa ustawi wa serikali na jamii.

Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Karagwe, Jeneroza Kaijage na Asteria Exsavery, wameliomba shirika hilo kutoa kipaumbele kwa wanafunzi waliopo kwenye wilaya hiyo na kwamba itapunguza wimbi la mabinti kuolewa katika umri mdogo na wengine kupelekwa mjini kufanya kazi nyumbani.



Mafundi wakichimba mashimo kwa ajili ya kuweka uzio ili kuzuia watu wasikatishe katikati ya barabara ya Morogoro, eneo la Ubungo Mataa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wasaidizi kisheria wawezeshwa

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA linalofanya kazi ya kukuza upatikanaji wa haki nchini kupitia uwezeshaji wa kisheria la Legal Services Facility (LSF) kwa kushirikiana wadau mbalimbali na mashirika zaidi ya 200 ya wasaidizi wa kisheria, limetoa elimu ya masuala ya kisheria iliyowafikia watu takribani milioni 6.4 mwaka jana.

Uongozi wa shirika hilo umesema kuwa kati yao, asilimia 45 ni wanaume na asilimia 55 ni wanawake.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alibainisha hayo jijini Dar es Salaam jana wakati akifungua mkutano wa siku mbili uliofanyika kwa njia ya mtandao kwa lengo la kukutana na wadau wake ambao ni mashirika zaidi ya 200 ya wasaidizi wa kisheria nchi nzima.

Alisema lengo la mkutano huo ni kujadili masuala ya kiutendaji katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria kwa makundi yenye uhitaji hususani wanawake na watoto.

"Tumekuwa tukifuatilia kwa karibu kazi zinazofanywa na wadau wetu. Tunatumia taarifa hizi kwa ajili ya kupanga mikakati mizuri ili kuweza kuwafikia watu wengi hasa wenye uhitaji kama vile wanawake na watoto.

"Lengo letu ni kuleta maendeleo kwa kuwa tunaamini kabisa hakuna maendeleo bila haki. Nina furaha sana kuonana nanyi leo. Ingawaje mko mbali, lakini kupitia teknolojia tunaweza kukutana na kujadili masuala muhimu katika mustakabali mzima wa upatikanaji wa haki.


MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD
P.O. Box 61424 DAR ES SALAAM, TANZANIA
TELL: 0787129539/0719656930
Dealers in: Auctioneer & Debt collection
Email: mabundacompanyltd@gmail.com

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na BUBALE LIMITED tutauza kwa mnada wa hadhara vifaa vilivyotajwa hapo chini kuanzia tarehe 10/03/2021 na kuendelea baada ya kutoka kwa tangazo.

1. Harvest Class CS228
2. Tractor Massey Fergusson 9240
3. Tractor Massey Fergusson 9240 - as it is stands
4. Trailer 18 t
5. Crops sprayer Nodet
6. Planter Kinze 3650 – 16/31
7. Fertilizer sprayer 24m Amazon
8. Ripper / per ripper
9. Crusher
10. Bulldozer Caterpillar D5 LPG
11. Bulldozer Caterpillar D5 LPG - as it is stands
12. Excavator 10 t Case

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada kurudiwa.
4. Taratibu za kuona au kukagua vifaa, zitafanyika tarehe 01/03/2021 kabla ya kufanyika kwa mnada

Kwa mawasiliano zaidi
0787129 539/0655 129 539
Email: mabundacompanyltd@gmail.com


# Buzwagi, Bulyanhulu zapata cheti cha usafi wa mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Barrick Gold imesema inazingatia kwa makini suala la utunzaji wa mazingira na ndiyo sababu migodi yake ya Buzwagi na Bulyanhulu imepatiwa vyeti vya utunzaji wa mazingira kwa ubora wa viwango vya kimataifa.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Dk. Mark Bristow, wakati akitoa mada kwenye kongamano la kimataifa la madini.

Kongamano hilo la kimataifa lililowashirikisha wachimbaji wadogo na wakubwa kutoka nchi tisa duniani lilifunguliwa rasmi jana na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Dk. Bristow alisema hadi kufikia kipindi cha nne cha mwaka huu, kampuni hiyo itahakikisha mgodi wa North Mara nao unaingizwa na kutambuliwa kimataifa kwa ubora wa utunzaji wa mazingira ili kuhakikisha migodi yote ya Barrick inatunza mazingira kwa viwango vya kimataifa.

Alisema tangu ianze shughuli zake, kampuni hiyo imefanikiwa kutimiza ahadi zake kwenye usimamizi wa maji na imepata mafanikio makubwa kwa kuboresha mtambo wake wa kusafisha maji.

Alisema wameongeza uwezo wa kusafisha maji kutoka wastani wa lita milioni 2.5 hadi kufikia lita milioni 28.6 kwa siku na kwamba wakati wanachukua mgodi wa Acacia ulikuwa kwenye hali mbaya sana, lakini wamefanikiwa kuuboresha.

Kuhusu mgodi wa North Mara, alisema umekuwa mgodi wa uchimbaji chini ya ardhi katika kipindi cha mwaka mmoja na wamefanya maboresho makubwa kuhakikisha shughuli za uchimbaji zinafanyika kwa ufanisi mkubwa.

Alisema ili Barrick iendelee kuwa kampuni bora wameendelea kuwekeza kwenye teknolojia ya hali ya juu na ili kushindana kwenye sekta hiyo ya madini kulinganisha na mataifa mbalimbali.

"Tunaamini kuna fursa nyingi kwa vijana wa Tanzania tunapowatafuta wale wenye vipaji wafanye kazi kwenye migodi yetu na migodi yetu imeendelea kuzalisha dhahabu nyingi kwa kufuata mwongozo wetu wa mwaka 2020 na kumekuwa na maboresho makubwa mwaka hadi mwaka," alisema.

Alisema wamepata mafanikio makubwa tangu wachukue mgodi wa Acacia na Mgodi wa Nortn Mara umezalisha kwa kiasi kikubwa kulinganisha na migodi mingine ya kampuni hiyo.

Alisema shughuli za utafutaji madini katika mgodi wa Bulyanhulu zinaonyesha mafanikio makubwa na inaonyesha mgodi huo utakuwa wa kimataifa.

# Askofu atoa neno magonjwa tishio

**Na Gurian Adolf, NKASI**

ASKOFU wa Kanisa la Moraviani Jimbo la Sumbawanga mkoani Rukwa, Conrad Nguvumali, amewata waumini wa kanisa hilo kuchukua hatua zinazostahiki katika kujikinga na magonjwa ya kuambukiza kama homa kali ya mapafu Covid-19 kwa kuwa magonjwa haya si pepo kama wengi wanavyodhani.

Akizungumza kwenye ibada ya Jumapili katika Kanisa la Moravian Usharika wa Namanyere wilayani Nkasi, alisema waumini wengi wanaomwamini Mungu wameuchukulia ugonjwa wa homa ya mapafu ni pepo na kujikita kwenye kumwomba Mungu tu na kuacha kuchukua tahadhari za kitaalamu za kujikinga na maradhi hayo ya kuambukiza.

Alisema magonjwa haya mapya jamii inaweza kujikinga nayo kwa kufuata maelekezo ya kitaalamu kama ilivyo katika magonjwa mengine kama kipindupindu, malaria na mengineyo, badala ya kujifungia ndani kufanya maombi ya kumuomba Mungu bila ya kuchukua tahadhari.

"Wameibuka Wakristo wenye imani kali, ambao wanasema kuwa magonjwa haya yaliyopo ni pepo, huku wakiamini katika maombi pekee na kuacha kufuata kanuni za afya juu ya kukabiliana na maradhi hayo, kitu ambacho si sawa... pamoja na kumuomba Mungu pia wafuate maelekezo ya wataalamu wa afya," alisema.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kutodharau maelekezo ya kitaalamu, kwa kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya kukabiliana na maradhi haya hatari, ingawa pia hawanabudi kumwomba Mwenyezi Mungu ili kutuepusha balaa la magonjwa hayo hatari.

Mchungaji wa Kanisa hilo, Joel Kalinga, alisema Mungu alimuumba mwanadamu na kumpa ujuzi, hivyo ni lazima ayatumie maarifa hayo katika kukabiliana na magonjwa hayo, huku akiendelea kumwomba Mwenyezi Mungu.

# Waliozozania SUA wasuluhishwa

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MGOGORO wa muda mrefu wa kugombania Shule ya Sekondari ya SUA, Kata ya Mbuyuni na ya Magadu katika Manispaa ya Morogoro, umemalizika kwa kila kata kupewa kazi ya kujenga madarasa.

Katika mvutano huo wa siku nyingi ambao, kila kata ilidai kuwa shule hiyo ni mali yake, ulitatuliwa kwa namna tofauti na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, kuwatwisha mzigo watendaji wa mitaa ya kata hizo kujenga vyumba vitano vya madarasa ndani ya mwezi mmoja. Uamuzi wa Ole Sanare, umekuja baada ya kuzuru kata hizo na kushuhudia kuwa hakuna ujenzi wa madarasa, kwa kisingizio kuwa hafahamiki mmiliki halali wa sekondari ya SUA.

Baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili na kujiridhisha, Mkuu wa Mkoa alieleza kuwa mvutano huo hauna tija kwa wanafunzi wanaohitaji kuingia madarasani yanayotakiwa kujengwa haraka ili waanze masomo.

Aliwaagiza watendaji wa mitaa wa kata zote mbili kusimamia ujenzi huo.

Katika maagizo yake alitoa mwezi mmoja kujenga vyumba vitano vya madarasa pembeni mwa majengo ya shule, lakini ndani ya eneo lake ili kukamilisha haraka kukabiliana na changamoto ya upungufu wa madarasa katika shuleni hapo.

Ole Sanare, alisema Kata ya Mbuyuni yenye mitaa sita itajenga vyumba viwili wakati Magadu yenye mitaa tisa itajenga vyumba vitatu vya madarasa na kuwezesha kupatikana vyumba vitano.

"Natoa mwezi mmoja kwa kila kata kujenga vyumba hivyo tulivyowapangiana na vifikie usawa wa linta. Ninataka yakikamilika mumkabidhi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ili kuyamalizia," alisema. Kuhusu mvutano uliokuwapo, mkuu huyo wa mkoa aliwataka viongozi wa pande zote mbili kukubaliana kujenga madarasa hayo matano mbali kidogo na majengo ya sasa ya shule hiyo na yatakapokamilika siku zijazo kupitia majengo hayo wanaweza kuamua kuifanya shule inayojitegemea, hivyo kila kata kuwa na shule yake na kuondoa mvutano uliokuwapo.

Diwani wa Kata ya Mbuyuni, Samwel Msuya, alisema changamoto iliyokuwapo katika ujenzi wa sekondari ya SUA, ni baada ya kata yake ya Mbuyuni kushtakiwa na kukatazwa kuendeleza shule hiyo, hali iliyosababisha kudorora kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Msuya alisema hadi sasa changamoto hiyo imekwishatatuliwa na wananchi wa Mbuyuni na Magadu wapo tayari kuendeleza ujenzi wa madarasa katika shule hiyo.

Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga, alisema, umiliki wa shule hiyo iwe ya nani siyo muhimu kwao.

Aliwaambia kinachotakiwa ni kujenga madarasa ili watoto waliokosa nafasi ya kusoma waingie madarasani na kuanza kusoma na kwamba wahusika wakuu wa kujenga madarasa hayo ni wenye watoto ambao ni wazazi wanaoishi katika kata hizo.

Aliwataka washirikiane kutekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa la kujenga madarasa hayo matano.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya CCECC, wakiendelea na ujenzi wa kituo kipya cha mabasi ya mwendokasi, katika eneo lililokuwa stendi ya mikoani, Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanahabari wahimizwa kuchochea maendeleo

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

VYOMBO vya habari vimekumbushwa kutambua nafasi yao katika maendeleo ya taifa na kusaidia kufanikisha jitihada za serikali za kufikia uchumi wa viwanda kwa kuandika taarifa zitakazosukuma agenda muhimu.

Akifungua semina ya wana habari za uchumi, biashara na fedha jana mjini Mtwara, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Julian Banzi, alisema wajibu wa vyombo hivyo ni kuelezea mipango ya kuelekea uchumi wa viwanda, changamoto na namna ya kuzitatua.

Kaimu Mkurugenzi wa BoT, Mtwara, David Mponeja, akisoma hotuba kwa niaba ya Banzi, aliwataka waandishi kujua kuwa maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi ambayo ikikamilika itachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi.

Aidha, aliwataka kufahamu jinsi kila mmoja anavyoweza kuchangia uchumi kusonga mbele.

"Kwa mfano, tumieni weledi wenu kuwafahamisha wananchi hatua mbalimbali ambazo serikali inazichukua katika kuwatumikia, msiache kuwaeleza hatua ambazo miradi ya kimkakati kama reli ya kisasa, mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga na ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme katika Mto Rufuji umefikia na faida ambazo taifa litapata," alisema na kuongeza:

"Kufanya hivyo ni kuwajibika, ndiyo uzalendo. Maendeleo ya taifa letu yanawategemea sana ninyi kutekeleza majukumu yenu kwa uadilifu, weledi na uzalendo kwa taifa lenu."

Kadhalika, Banzi alisema makala za sekta mbalimbali kama benki na taasisi za fedha, uchumi, huduma za bima, afya, kilimo, ujenzi pamoja na mifano mbalimbali ya watu na kampuni zinazojishughulisha na kazi hizo ni kichocheo kwa wengine kupenda kujishughulisha.

"BoT inafurahi kuona miaka ya hivi karibuni vyombo vingi vya habari vimekuwa vikitenga muda na kurasa maalum kutangaza habari za uchumi, biashara na fedha," alipongeza Banzi.

Awali, mwenyekiti wa chama hicho, Abduel Elinaza, alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kuwajengea uwezo wanahabari kuandika taarifa za kina za masuala ya fedha, uchumi na biashara.

# GGML mshindi wa jumla sekta ya madini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited imeibuka mshindi katika vipengele vitatu muhimu na mshindi wa jumla wa kampuni inayofanya vizuri katika sekta ya madini mwaka 2019/2020.

Tuzo hizo zimetolewa na serikali kwenye mkutano wa kila mwaka wa madini na uwekezaji katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Katika tukio hilo, ambalo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, GGML imetambuliwa kwa mchango wake katika sekta ya madini na ukusanyaji wa mapato ya serikali, utendaji mzuri katika masuala ya mazingira na usalama sanjari na utekelezaji mzuri wa miradi ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii kwa mwaka 2019/2020.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hizo, Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo, alishukuru serikali kwa kutambua mchango wa GGML na kuahidi kuendelea kufanya kazi na wadau wote katika sekta ya madini ili kufikia malengo ya serikali na kuongeza mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa.

"Kuibuka mshindi katika vipengele vya kodi, mazingira na usalama sanjari na utekelezaji mzuri wa miradi kwenye jamii inayotuzunguka ni ushuhuda wa dira ya kampuni yetu ambayo ni kuwa kampuni ya kwanza ya madini duniani. Tuzo hizi zinatambua pia mchango wetu kama washirika muhimu wa maendeleo kwenye Serikali ya Tanzania pamoja na tunu zetu muhimu za kuhakikisha jamii inayozunguka mgodi inafaidika kutokana na shughuli zetu," alisema Shayo.

"Kwa miaka 21 iliyopita, kampuni ya GGML imekuwa mshirika muhimu wa kusaidia jitihada za serikali ya Tanzania katika kuboresha sekta ya madini ikiwamo michakato ya kushirikiana na kujadiliana ambayo imekuwa ikichochewa na Wizara ya Madini," alisema.

Alisema GGML itaendelea kufanya kazi na serikali ili kufikia malengo ya serikali ya kuhakikisha sekta ya madini inachangia zaidi ya asilimia 10 ya pato ghafi la taifa ifikapo mwaka 2025.

Mwaka huu GGML walikuwa mojawapo pia ya wadhamini wakuu wa mkutano huo wa siku mbili ambao umemalizika Februari 23, 2021.




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi tuzo Makamu wa Rais wa Kampuni ya GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo, baada ya kampuni hiyo, kuibuka mshindi katika vipengele vitatu muhimu na mshindi wa jumla wa kampuni inayofanya vizuri katika sekta ya madini mwaka 2019/2020. **MPIGAPICHA WETU**

# WMA yaonya wafanyabiashara wanaokiuka sheria

**Na Richard Makore, MWANZA**

WAKALA wa Vipimo (WMA), Mkoa wa Mwanza, umewaonya wafanyabiashara wanaokiuka sheria na kuharibu mizani ama kujaza mizigo kupita kiasi ikiwamo magunia ya 'Lumbesa'.

Umesema kwamba watakaobainika watakabiliwa na adhabu ya kulipa faini ya Sh. milioni 50.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Meneja wa WMA mkoni Mwanza, Balisco Kapesa, alisema sheria ya vipimo inawataka kutoza faini kama hiyo pamoja na kutaifisha chombo ikiwamo gari itakayokutwa imebeba mizigo isiyoruhusiwa kisheria.

Alisema sambamba na kutoza faini hiyo, WMA kupitia maofisa wake wanatoa elimu kwa jamii wakiwamo wakulima na wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kutumia mizani katika kununua na kuuziana vitu.

Alisema wafanyabiashara wanatumia vipimo vya Lumbesa kuwaibia wakulima na kwamba WMA imejua hilo na inawatumia maofisa wake kwenda kutoa elimu.

Hata hivyo, alisema kuwa mizani za kisasa 'digital' zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza wizi uliokuwa unafanywa na wafanyabiashara kwa kuwa yote imekaguliwa na kuwekewa alama maalum na WMA.

Aliitaka jamii kuendelea kutoa ushirikiano na taarifa wanapohisi kuibiwa kupitia mizani ili WMA iweze kuchukua hatua za haraka kumaliza tatizo hilo.

## Madiwani wataka uchunguzi wanawake, vijana mikopo

**Na Happy Severine, BUSEGA**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, wametaka vikundi vya vijana, wenye ulemavu na wanawake kufanyiwa uchunguzi wa kina kabla havijapewa mikopo.

Walisema vikundi hivyo vichunguzwe kama vinafaa kupewa mikopo na kama vipo halali ili kupunguza changamoto iliyopo kwenye halmashauri hiyo kwa baadhi ya vijana kupewa mkopo kisha kugawana.

Walisema hayo juzi na kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Halmashauri, siku chache tangu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kubaini madudu kwa vikundi vilivyopewa mikopo.

Taasisi hiyo ilibaini uwapo wa vikundi hewa ambavyo vilipewa mkopo na halmashauri hiyo, huku vingine wanufaika wakigawana fedha bila ya kutekeleza mradi walioombea mkopo na vingine vikikutwa havina ofisi.

Diwani wa Kiloleli, Vumi Magoti, alisema tatizo kubwa lipo kwenye ofisi ya maendeleo ya jamii ambao wameshindwa kuvikagua vikundi ambavyo vimekuwa vikileta maombi kwao ya kupewa mikopo.

Mbunge wa Jimbo hilo, Simon Songe, aliviomba vyombo vya ulinzi na usalama katika wilaya hiyo ikiwamo TAKUKURU kusaidia katika ku-,vichunguza vikundi ambavyo vina-'leta maombi ya kupatiwa mikopo.

## Walalamika taka kwenye vizimba

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WAKAZI wa Majengo Makaburini katika Manispaa ya Shinyanga, wamelalamikia uchafu kwenye vizimba vya kukusanyia takataka katika makazi yao.

Wamesema uchafu huo unahatarisha afya zao na kuhofia kupata magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Walipaza kilio chao jana wakati Nipashe ilipotembelea maeneo hayo na kushuhudia kizimba hicho kikiwa kimeja uchafu.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo jirani na kizimba hicho, Bakari Saidi, alisema mvua zinaponyesha uchafu hupelekwa na maji kwenye maeneo ya makazi yao na kusababisha harufu mbaya.

"Tunaomba utusaidie kupaza sauti kwa mamlaka husika, afya zetu zipo hatarini ikiwamo kupata magonjwa ya mlipuko, uchafu huu unafika mahala una zagaa kwenye makazi yetu na watoto kuanza kuuchezea," alisema Bakari.

"Hata Meya wa Manispaa ya Shinyanga alishapita hapa na kujionea hali halisi, tukajua kwamba uchafu huu utazolewa muda si mrefu, lakini hali bado iko vilevile na kipindi hiki cha mvua sidhani kama tutapona kweli tunaomba msaada jamani uchafu uzolewe," aliongeza.

Naye Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, alisema alishapita kukagua maeneo yote yenye vizimba na kutoa maelekezo uchafu huo uzolewe haraka hata kwa kukodi magari ili kulinda afya za wananchi.

‘DPP Fatou Bensouda, sasa kung’atuka ICC’



Ukurasa 12



Ukurasa 13

**Mtihani nani ni nani 2025**


# siasa

JUMATANO FEBRUARI 24, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

**Kijazi ameondoka, akilijaza mema taifa**

# Umaarufu wa Maalim Seif umedumu kwa sababu...

## •Inakuwaje miaka 30, asiandae wa kuvaa viatu vyake?

**Na Sabato Kasika**

LEO ni wiki moja tangu Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) ilipompoteza Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki dunia Februari 17.

Kifo chake kilihitimisha safari ya kisiasa ya mwanasiasa huyo mashuhuri aliyejizolea sifa lukuki visiwani Zanzibar, kutokana na jinsi alivyokuwa amebeba siasa za upinzani kwa miaka 30.

Maalim Seif amefariki dunia akiwa ametumikia wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais ndani ya siku 100 baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo mwanzoni mwa Desemba, mwaka 2020.

Itakumbukwa kuwa kiongozi huyo alidumu kwa muda mrefu akiwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) kabla ya kuibuka mgogoro wa kiuongozi, katika chama hicho, uliosababisha aondoke na kujiunga na Chama cha ACT-Wazalendo.

### MWASISI KAMAHURU

Kabla ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, kulikuwa na vuguvugu la kutaka mageuzi, huko visiwani Zanzibar na kulikuwa na Kamati ya Kupigania Mageuzi na Uhuru wa Zanzibar (KAMAHURU).

Waanzilishi wa vuguvugu hilo walikuwa ni Maalim Seif na baadhi ya wenzake waliofukuzwa CCM wakiwamo Shaban Mloo, Hamad Rashid Mohamed, Maulidi Makame, Ali Haji Pandu, Khatib Hassan, Soud Yusuf Mgeni na Ali Salim.

Baadaye Maalim Seif aliwekwa kizuizini na alipotoka, alishauri KAMAHURU iungane na “Civil and Legal Rights Movement” ya Tanzania Bara, ambapo waliungana na kuzaliwa CUF iliyomaanisha “Civic United Front.”



Aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad. **PICHA: MTANDAO**

Civic United Front ambayo baadaye ilikuja kuwa Chama cha Wananchi (CUF), ilikuwa ikiongozwa na James Mapalala ambaye alichaguliwa kuwa wa chama hicho, huku Shaaban Mloo akiwa Makamu Mwenyekiti.

Maalim Seif alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu, na alishikilia wadhifa huo kwa zaidi ya miaka 20 chini ya Mapalala, na hata Mapalala alipoondolewa katika chama mwaka 1994 na kuchaguliwa Prof. Ibrahim Lipumba, Maalim Seif aliendelea kuchaguliwa katika nafasi hiyo.

Aliachia nafasi hiyo ya ukatibu mkuu Machi mwaka 2019 baada ya kuondoka CUF na kujiunga na ACT-Wazalendo na kuchaguliwa Mwenyekiti hadi alipofariki dunia wiki iliyopita.

### KUDUMU MUDA MREFU

Naibu Katibu Mkuu CUF, Magdalena Sakaya, anasema, Maalim Seif alikuwa kiongozi mwenye uzoefu mkubwa kisiasa kati ya viongozi wa upinzani, akianzia utumishi wa juu serikalini alipokuwa kijana.

“Uzoefu wake ulikuwa ni silaha tosha binafsi nilijifunza mengi kwake, alijiamini, jasiri na hakuwa mwoga, ndiyo maana aliaminika na kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu kila uchaguzi ulipofanyika,” anasema Sakaya.

Anafafanua kuwa Katiba ya CUF inaelekeza kwamba Mwenyekiti wa CUF atatoka Bara na Katibu Mkuu Visiwani, hivyo kutokana na msimamo usioyumba, aliendelea kuchaguliwa kwa kura nyingi.

“Tofauti zilizojitokeza ndani ya CUF kuzijadili, lakini ninaweza kusema kuwa msimamo, ujasiri na kutoyumba, ni mojawapo ya siri iliyomfanya adumu kwa muda mrefu katika nafasi ya Katibu Mkuu wa CUF hadi alipohama,” anasema.

Sakaya anasema, katika siasa, Maalim Seif amewahi kupitia kifungo cha kisiasa, kutokana na msimamo wake, lakini hakuyumba na badala yake akageuka kuwa shujaa na kujizolea umaarufu.

Mtu anayeweza kukaa gerezani kwa ajili ya demokrasia na akatoka kisha akaendelea kuipigania, inamjenga katika sifa ya uvumilivu na kutokata tamaa, ninadhani anafaa kuwa kiongozi,” anasema.

Anamwelezea kuwa kwa kipindi kirefu Maalim Seif amepambana na utawala wa CCM bila kuchoka wala kurudi nyuma na amesimama kidete na kuhakikisha masilahi ya wananchi wa Zanzibar yanalindwa.

“Kutokana na ushawishi wake katika siasa wa kutaka haki sawa kwa wote, ilifikia wananchi wa Zanzibar na hasa Pemba kukataa wawakilishi kutoka CCM bali wale wa chama ambacho Maalim Seif yumo,” anasema.

Naibu Katibu Mkuu huyo anasema, Maalim Seif ana mchango mkubwa katika kuimarisha upinzani usiyumbishwe na wasioutakia mema, na kwamba alikuwa hana mzaha.

### KOSA KIUFUNDI

Inaelezwa kuwa pamoja na kwamba alikuwa kiongozi mwenye msimamo na ushawishi mkubwa kwa Zanzibar, bahati mbaya hakuandaa watu wa kuvaa viatu vyake baada ya yeye kustaafu au kufariki dunia.

Hatua hiyo ya kutoandaa vijana wa kumrithi, inaweza kufuta upinzani visiwani Zanzibar, kwa madai kwamba hakuna mtu mwenye ushawishi kama alivyokuwa Maalim Seif.

INAENDELEA UK.14

UCHAMBUZI

# ‘DPP Fatou Bensouda sasa kung’atuka ICC’




Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, Fatou Bensouda. **PICHA: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA masuala ambayo yanagusa utetezi wa haki za binadamu na uendeshaji mashtaka ya kimataifa, hukosi kulifahamu jina, Fatou Bensouda, Mwendesha Mashataka wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC).

Mwanamama huyu ambaye pengine angeitwa ‘DPP’ kwa Tanzania, asili yake ni Gambia, amewahi kuwa Waziri wa Haki wa nchi hiyo na amefahamika duniani kutokana na uendeshaji wa mashtaka kimataifa.

Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai mwaka huu anamaliza muhula wake wa miaka 10 ifikapo Juni.

Kwa wengi hawatasahau kazi yake yapo mengi ambayo alikumbana nayo katika kazi yake, ikiwamo maswali tata na kutajwa kuziangazia pekee kesi za wakuu wa serikali za Afrika.

Fatou alimrithi, Luis Moreno Ocampo, anayetoka Argentina, mtangulizi wake huyo ni wakili, alichukuwa wadhifa huo baada ya kufanya kazi ICC kama Kaimu Mwendesha Mashtaka kuanzia mwaka 2004 hadi 2012.

> Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai mwaka huu anamaliza muhula wake wa miaka 10 ifikapo Juni.

**UZOEFU**

Nchini Gambia, alikuwa mwanasheria na msomi aliye na Shahada ya Uzamili wa Sheria ya Kimataifa ya Shughuli za Baharini.

Mwanamama huyu alijijengea uzoefu mapema akishauri masuala ya kisheria kwenye jopo la mahakama inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN), ambayo iliwahukumu viongozi wakuu wa mauaji ya kimbari, nchini Rwanda.

Baada ya wajumbe wa nchi wanachama wa ICC kukutana mjini New York, Marekani na kumchagua mwendesha mashtaka anayemrithi Fatou, mstaafu huyo, atakuwa anakamilisha muhula wake.

**MRITHI WA FATOU**

Wagombea tisa, walijitokeza kuwania wadhifa wa mwendesha mashtaka wa ICC wakiwamo majaji wawili kutoka Nigeria na mwingine Uganda.

Mshindi wa nafasi hiyo anayemrithi Fatou amekwishapatikana ni Karim Khan (50) wakili kutoka Uingereza, aliyekuwa kati ya wagombea tisa.

Wengine waliogombea ni Robert Petit, mwendesha mashtaka kutoka Canada, Jaji Susan Okalany (Uganda), Jaji Morris Anyah (Nigeria), Fergal Gaynor ambaye ni mwendesha mashtaka kutoka Ireland.

**KAZI ICC**

Kwa vipindi tofauti, Fatou aliwatia hatiani washtakiwa kadhaa ikilinganishwa na Moreno.

Hivi karibuni alisema mwasisi wa zamani wa Uganda, Kamanda Dominic Ongwen, amekutwa na hatia za uhalifu wa kivita na kuhukumiwa, pia aliwahi kutoa mashtaka yaliyowakabili Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta na aliyekuwa Rais wa Sudan Omar al-Bashiri.

Kitendo hicho, baadhi ya viongozi wa nyadhifa tofauti kutoka barani Afrika na duniani, walimkosoa wakidai kwamba, DPP huyo anang’ang’ania kufuatilia uhalifu unaojiri Afrika ingawa ICC ina nchi wanachama 123 hadi kufikia mwaka jana, ambako pengine kuna uhalifu kama huo.

ICC ilimshtaki Al-Bashir (75) kwa makosa ya uhalifu wa kivita na mauaji ya halaiki katika mgogoro wa Darfur uliojitokeza miaka ya 2000.

Licha ya Al-Bashir kuwa na mashtaka mengine nchini mwake na kukutwa na hatia ya makosa ya utakatishaji fedha, rushwa, alikutwa na fedha nyingi za ndani na za kigeni pamoja mali bila hati za umiliki na kumhukumu kifungo cha miaka miwili, Sudan ilikataa kumpeleka ICC.

**KAMANDA LRA**

Pia, ICC, mwaka huu imemkuta na makosa ya uhalifu wa kivita na kumtia hatiani, mbabe wa zamani wa kivita wa kundi la Lord’s Resistance Army (LRA) la Uganda, Dominic Ongwen.

Hukumu ilisomwa na Jaji Bertram Schmitt, na kusema “hatia yake imepatikana bila ya kuwa na mashaka yoyote.”

Hukumu hiyo ya ICC ni baada ya kesi hiyo kuendeshwa zaidi ya miaka minne tangu mwaka 2016.

Ongwen katika mashtaka 70, anayodaiwa kufanya uhalifu dhidi ya binadamu, na kundi la waasi la LRA, likongozwa na Joseph Kony, mwaka 2000, ambaye hata hivyo hajapatikana na kufikishwa ICC..

Katika utetezi wake, Ongwen amejitetea na akiapa kwa jina la Mungu kwamba hana hatia, mawakili walisema mashtaka dhidi yake yaondolewe kwa kuwa mbabe huyo wa kivita aliathiriwa kisaikolojia baada ya kuchukuliwa mateka na waasi alipokuwa mtoto.

**VIONGOZI KENYA**

Mwendesha Mashtaka Fatou alitaka ushahidi zaidi kwenye kesi iliyomhusisha Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, kwa mashtaka ya ghasia zilipoteza maisha ya watu kadhaa, baada ya uchaguzi katika mwaka wa 2007 hadi 2008.

Septemba 9, mwaka 2014, ICC ilimtaka Kenyatta kufika mahakamani kwa madai kwamba serikali yake inazuia nyaraka zinazotakiwa na mwendesha mashataka.

ICC ilikataa ombi la Mwendesha Mashtaka ICC, Fatou kuahirisha kesi dhidi ya Kenya na kumpa wiki moja kutupilia mbali kesi hiyo au atoe taarifa mahakamni kwamba, amepata ushahidi wa kutosha kuendelea na kesi hiyo.

Majaji wa mahakama walikataa hoja ya Fatou kwamba serikali ya Kenya imekataa kutoa ushirikiano.

Alikiri kwamba hana ushahidi wa kutosha, aliomba muda ili aendelee kutafuta ushahidi, baada ya mashahidi aliokuwa nao kuamua kujiondoa katika kesi hiyo, huku akiituhumu serikali ya Kenya kukataa kutoa ushirikiano.

**LAURENT GBAGBO**

Kesi ya ICC dhidi ya aliyekuwa Rais wa Ivory Coast, Laurent Gbagbo, Januari 28, mwaka 2016, mwendesha mashtaka huyo katika kesi hiyo iliyowasilishwa Novemba 30, mwaka 2011, mashtaka manne yalithibitishwa ikiwamo uhalifu dhidi ya ubinadamu, ikiwamo mauaji, ubakaji na vitendo vingine vya kikatili, vikiwa ni jaribio la kuua na utesaji.

Gbagbo alishtakiwa pamoja na Charles Blé Goudé, raia wa Ivory Coast, ambaye alikabiliwa na mashtaka hayo. **MITANDAO**

# Mtihani nani ni nani 2025

Na Joseph Kulangwa




Rais John Magufuli na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, wakati utakapofika ni miongoni wa wakuu wa chama wanaotarajiwa kuwaambia Watanzania nani ni nani 2025. **PICHA: MTANDAO**

MARA zote kila baada ya uchaguzi, kuna usemi mashuhuri kwamba mwisho wa uchaguzi mmoja ni mwanzo wa mwingine. Maana yake ni kwamba, maandalizi huanza sawia.

Uchaguzi mkuu wa Tanzania hufanyika kila baada ya miaka mitano na kwa utaratibu uliozoeleka, rais anayeondoka akiwa ametumikia mhula mmoja, ana fursa nyingine ya kugombea kwa ajili ya miaka mingine mitano.

Kihistoria, utaratibu huo tangu uanzishwe baada ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kumaliza kipindi chake cha miaka 24, haujawahi kukosewa, Rais akaongoza kwa muhula mmoja tu wa miaka mitano, kama ilivyotokea kwa Donald Trump wa Marekani hivi karibuni.

Rais John Magufuli mwaka jana, alichaguliwa tena kwa muhula wa pili na wa mwisho wa miaka mitano na ifikapo mwaka 2025, atatoa fursa kwa mwingine kuongoza nchi.

Kwa kawaida, kipindi ambacho rais mpya hutarajiwa, huwa kina mvutano miongoni mwa wanasiasa na wafuasi. Hivyo, kwa kulibaini hilo, ni dhahiri vuguvugu limeshaanza chini chini, kwa kuwa lango litakuwa wazi.

Hata hivyo, kwa hali ilivyo, kinyang'anyiro kitaweza kuwa kigumu zaidi, kutokana na ukweli kwamba mwelekeo uliopo, bado hakuna picha ya wa kumrithi Rais Magufuli, ambaye tayari ameshatangaza kutoongeza muda, mgombea anayemtaka asiwe anamzidi umri wakati ukifika.

Huo nao ni mtihani, kwamba kwa watakaokuwa wanamzidi umri Rais Magufuli, ifikapo mwaka 2025, hawatakuwa na nafasi ya kuingiza mguu kwenye kinyang'anyiro hicho, isipokuwa kama wazo hilo litabadilika.

Huko nyuma ilikuwa rahisi kutabiri nani atagombea urais na hata kuchaguliwa, ili mradi anatokana na CCM. Hiyo ilitokana na mchango wa sifa kihistoria alizokuwanazo mtarajiwa, kiasi kwamba hata wengine walijiweka kando baada ya kuzibaini.

Ilikuwa hivyo, kwa Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ambaye aliweka historia ya kujiuzulu uwaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kutokana na kashfa ya mauaji ya mahabusu mkoani Shinyanga, lakini kuiongoza Zanzibar akiwa Rais kwa mafanikio.

Pia ilitokea kwa Benjamin Mkapa, ambaye akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, alishiriki katika majadiliano muhimu ya kimataifa yaliyoihusisha Tanzania na kuipa sifa, ikiwa ni pamoja na siasa za Kusini mwa Afrika.

Mkapa alihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa umahiri mkubwa na kueleweka.

Tanzania iliheshimika kimataifa, kutokana na uongozi wa Nyerere na hata Mkapa akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, ambapo alisikilizwa kila alipowasilisha hoja katika mikutano mikubwa ya kimataifa.

Jakaya Kikwete, akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, aliendeleza alipoachia Mkapa, kwa kuitangaza Tanzania na kuitetea katika medani ya kimataifa, huku akihudhuria mikutano mingi ya kimataifa akimwakilisha Rais Mkapa na kote aliheshimika hata kuwasilisha mada na hoja katika vyuo vikuu vya kimataifa.

Mbali na hiyo, Kikwete licha ya kufahamika ndani ya chama chake, lakini hata mitaani aliheshimiwa na kupendwa, kutokana na alivyojishusha na kuwa karibu na watu.

Rais Magufuli pia, akiwa Waziri wa Ujenzi chini ya Rais Mkapa, alijizolea sifa ya uthubutu na umakini utekelezaji kazi zake, hata kufikia hatua Mkapa kumpa sifa ya askari wa mwavuli, akidhibiti magari ya serikali yaliyokuwa yakitumiwa ovyo.

Ni Rais Magufuli, aliyekuwa akikagua ujenzi wa barabara na kuhenyesha makandarasi waliokuwa wakitekeleza majukumu yao chini ya viwango. Alitembea vifaa kukagua viwango vya unene wa lami.

Akiwa Waziri aliyesimamia uvuvi, alikamata meli ya uvuvi ya kigeni ikivua samaki kwa njia haramu katika bahari kuu ya Tanzania na kufanya dunia kutambua jinsi taifa linavyolinda raslimali zake, ili kujenga zingine kwa ajili ya viongozi.

Rekodi hizo zilisababisha viongozi hao kuingia kirahisi kwenye kinyang'anyiro cha urais na kushinda huku siri kubwa ikiwa ni kwamba ili uingie kwenye mbio sharti upate kuwa waziri huko nyuma.

Hii ndiyo iliyotokea kwa Mwinyi, Mkapa, Kikwete na sasa Magufuli.

Mtu atajiuliza hivi, je, nani atakuwa nani ifikapo mwaka 2025? Je, kutakuwa na uwezekano wa kupata rais ambaye hatakuwa na historia ya kuwa waziri? Inawezekana. Lakini sifa hiyo itakuwa imebebwa na kigezo kipi? Lazima kiwe cha utendaji kazi uliotukuka, ambao ikiwezekana uzidi wa viongozi hao waliotangulia.

Hivi sasa kwa jicho la haraka, ni mtihani mzito kumwona mtu ambaye atavaa viatu hivyo, baada ya Rais Magufuli kuvivua Oktoba 2025?

Kwa kuwa suala la 'atake asitake, tumlazimishe' halitakuwapo kwa mujibu wa msisitizo wake.

Baadhi ya viongozi wanaomsaidia Rais Magufuli hivi sasa, wameshindwa kumsoma na kufuata nyayo zake ambazo pengine zinaweza kuwasaidia au kuwaangusha, katika kinyang'anyiro cha 2025, au kwa kushindwa kwenda na kasi yake au kuizidi.

Inawezekana, wapo baadhi ya viongozi wanaogopa kutekeleza majukumu yao, wakihofia kuharibu na hatimaye kutumbuliwa. Hao wanalinda matumbo yao, hawapo kwa ajili ya kusaidia wananchi, licha ya Rais kuwaambia "tekeleza ukosee ukimsaidia mwananchi kuliko kusubiri mpaka Rais nije".

Wapo wanaotekeleza na kuzidi hadi kujiharibia, kwa kudhani wanamfurahisha kumbe wanakosea. Ndiyo hao wanaofikia hatua ya kujichukulia sheria mkononi na kukosesha vyombo vya sheria haki ya kutenda haki.

Wote wanaoyafanya hayo, si tu wanawakosea wananchi, lakini wanajipora sifa za kuaminiwa kupewa fursa ya kugombea na kushinda urais mwaka 2025. Kutajwa vizuri, kunatokana na mchango wa mhusika katika kusaidia wananchi.

> "Mbali na hiyo, Kikwete licha ya kufahamika ndani ya chama chake, lakini hata mitaani aliheshimiwa na kupendwa, kutokana na alivyojishusha na kuwa karibu na watu.

Ikumbukwe, nje ya CCM alipata kutokea Waziri Augustine Mrema, ambaye akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri Mkuu wa Serikali ya CCM, kisha baadaye akahamishwa kuwa Waziri wa Kazi na Vijana.

Ndio hapo alijitoa CCM, akiwa na rekodi hasa katika wizara ya mwanzo, alifanya makubwa kwa jamii kiasi cha kuaminika kuwa angeweza kuwa Rais mzuri mwaka 1995 pale alipovaa kofia ya upinzani, akipambana na Mkapa na wengineo.

Lakini, zamani kabla ya hatua hiyo, urais wa Tanzania ulikuwa unatoka kwa utaratibu wa zamu kati ya Tanzania Bara na Visiwani. Wapo ambao katika jicho la kisiasa walimmulika Waziri Mkuu, Edward Sokoine, kwamba huenda asingepoteza maisha mwaka 1984, angeingia katika orodha za wale huenda wangepokea kijiti kwa Mzee Mwinyi.

Sokoine anakumbukwa kwa vita vyake dhidi ya uhujumu uchumi, ambavyo alisababisha wafanyabiashara waliokuwa wamehodhi fedha, kuzitoa huku wengine wakitupa mali zao baharini kuchelea kukamatwa kutokana na jinai hiyo.

Hivyo, kama zamu hiyo ingeendelea, majina mengine maarufu yanayotajwa ndani ya mtiririko huo wa zamu, tukitafakari nani wa kuingia 2025.

***Siku njema.***

JUKWAA LA UONGOZI



Katibu Mkuu Kiongozi, John Kijazi wakati wa uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

# Kijazi ameondoka, akilijaza mema taifa

**Mwandishi Wetu**

JUHUDI za kuwavusha Watanzania kwenye umaskini, kuinua maisha yao na kulifikisha taifa kwenye uchumi wa kati ndilo ua la waridi analoliacha Katibu Mkuu Kiongozi, John Kijazi, likinukia kwenye bustani za taifa hili.

Licha ya kuwa mhandisi wa shahada ya uhandisi ujenzi (civil engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kisha kupata shahada ya uzamivu wa barabara kuu (highway engineering) nchini Uingereza, hakuwa mwanasiasa.

Kijazi aliyefariki wiki iliyopita, ametukuka na kuwa sehemu ya mafanikio makubwa Tanzania inayojivunia leo. Akiwa mshauri mkuu wa Rais na mtendaji mkuu anayesimamia utumishi na shughuli za umma, ataendelea kuishi.

Kijazi akiwa mshauri wa Rais John Magufuli, anakumbukwa kwa kufanikisha mambo makubwa kuanzia, elimu, ujenzi wa viwanda na miundombinu ambayo ni kazi zilizotukuka zinazoendelezwa na awamu ya tano.

Kijazi anakuwa daraja linalounganisha mafanikio ya awamu ya nne na ya tano na kuendelea kulifikisha taifa kwenye hatua za juu kimaendeleo zitakazoendelea kuishi kwenye vitabu vinavyozungumzia mafanikio ya Tanzania.

> “Mafanikio ya elimu hayaweza kutajwa bila kuzungumza kazi zilizofanywa na kiongozi huyo ambaye amefanikisha mambo yalifanyika serikalini.

Akiunganisha mafanikio hayo, Balozi Kijazi, aliendelea kusimamia utumishi wa umma kuboresha elimu na kuifanya ipae zaidi na kuwa na matokeo makubwa yanayoonekana kwenye jamii leo.

Awamu ya tano inapoingia madarakani ikiongozwa na Rais John Magufuli na Katibu Mkuu Kiongozi Kijazi, iliendeleza mengi kwenye sekta hiyo na kuachа mambo ya kujivunia.

Akiwa kiongozi wa makatibu wakuu na mkuu wa utumishi wa umma, halikadhalika Katibu wa Baraza la Mawaziri ambalo Rais ni Mwenyekiti, Balozi Kijazi, amefanya makubwa ambayo hayatasahaulika, licha ya kwamba Watanzania wengi hawamfahamu.

Katibu Mkuu Kiongozi, siyo mwanasiasa kwa hiyo hafahamiki kama walivyo wanasiasa wengine, lakini jukumu lake la kuwasimamia makatibu wakuu wote, linabakia kuwa ufanisi wake ndiyo unaoleta maendeleo kwenye sekta zote.

Kwa usimamizi na ufuatiliaji wake utendaji kazi serikalini, uchumi umepaa na kuifanya Tanzania kuingia kwenye uchumi wa kati.

Tukiangalia zaidi elimu ambayo inawahusu Watanzania wote, takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu katika awamu ya nne, zinasema serikali hiyo ilipoondoka madarakani iliacha shule za msingi 16,538.

Wakati huo wanafunzi katika shule hizo walikuwa 8,202,892 katika kipindi hicho.

Kwa upande wa sekondari awamu ya tano ilizikuta 4,753 na wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita walifikia milioni 1.7.

Kadhalika vyuo vikuu vilikuwa 49 na wanafunzi waliodahiliwa kwa takwimu za mwaka 2013/14 walikuwa zaidi ya 204,176.

Kwa kuangalia elimu pekee kuanzia Januari 2016, idadi kubwa ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza na wanaojiunga na kidato cha kwanza kwa shule za umma iliongezeka zaidi, kutokana na utekelezaji wa sera ya serikali kugharamia elimu, Kijazi aliyokuwa anaisimamia.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali zaMitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, anasema, idadi ya wanafunzi walioandikishwa iliongeza kutoka 10,201,972 mwaka 2015 hadi 12,034,599 mwaka 2020, kwa shule za msingi.

Aidha, kwa upande wa shule ya sekondari idadi ya wanafunzi wa awamu ya nne waliokuwa milioni 1.8 mwaka 2016, lakini leo wamefikia milioni 2.02 na kwamba tangu kuanza kwa utekelezaji wa kugharamia elimu serikali kuanzia Desemba 2015 hadi Juni, 2020, serikali imetumia Sh. trilioni 1.09 kugharamia elimu bila malipo.

Kijazi anahusika kuhakikisha kuwa hadi kufikia Juni 2020, mwaka huu, ujenzi wa shule mpya za msingi 905 ulikuwa umekamilika hivyo kuongeza idadi yake kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020, haikuwa kazi ndogo.

Kadhalika kwa ushauri uliotukuka aliotoa serikalini taifa limeongeza sekondari mpya 228 na hivyo kuongezeka kutoka shule 4,708 mwaka 2016 hadi 5,330 mwaka 2020.

Pamoja na ujenzi huo shule kongwe zimekarabatiwa na kuwekewa miundombinu mipya ili kuboresha elimu.

Mafanikio ya elimu hayaweza kutajwa bila kuzungumza kazi zilizofanywa na kiongozi huyo ambaye amefanikisha mambo yalifanyika serikalini.

Katika uongozi wake uchambuzi wa miswada, madokezo na ushauri mbalimbali umefanyika na kufanikisha kuanzishwa mamlaka za usimamizi ikiwamo TARURA, inayosimamia barabara kama TARURA inayohusika na barabara ndogo za mijini na vijijini wakati TANROAD inayosimamia barabara kuu.

Mamlaka nyingine ni Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) iliyoanza kazi 2019.

Licha ya kuwa mtaalamu wa miundombinu na barabara kazi zake nyingi zimefanikisha ujenzi wa Tanzania mpya ambayo wengi leo wanaifurahia.

Mhandisi Kijazi ameifanya Tanzania yote kufunguka na kuunganishwa kuanzia Tunduma, hadi Mwanza, Arusha, Tabora, Kigoma na mtandao wa barabara wenye lami na madaraja ya kisasa yamewekwa kila kulikokuwa na mito na madaraja duni.

Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mwanza ni mashuhuda wa madaraja na barabara zenye viwango na hadhi za kimataifa.

Ujenzi wa reli ya kisasa ya SRG inayojengwa kuanzia Dar es Salaam, Mwanza na kidogo ni matokeo ya uhandisi na ushauri uliotukuka wa Balozi Kijazi.

Ni ukweli kuwa serikali wakati wa Katibu Mkuu Kiongozi imefanya mambo makubwa mijini na vijijini na kwamba kuna vitu vingi ambavyo vimefanyika na la msingi ni kuvithaminisha na kuendelea kuvipa ubora na viwango

## Umaarufu wa Maalim Seif umedumu kwa sababu...

**INATOKA UK.11**

Mwanasiasa Thomas Ngawaiya anasema, ni lazima madhara ya kutokuwapo kwake yakuwa ni makubwa katika siasa za upinzani Zanzibar, kutokana na kinara wake kufariki dunia.

“Kwa miaka 30 ambayo amekuwa katika upinzani amefanya mengi, lakini bahati mbaya alifanya kosa la kiufundi la kutoandaa vijana wa kufuata nyayo zake, kwani sioni kama atatokea mtu kama yeye,” anasema Ngawaiya.

Anasema, kila anayefuatilia siasa za Zanzibar, anatambua nguvu na ushawishi wa kisiasa wa Maalim vilikuwa vikubwa na kwamba ndiye aliyeiua CUF pale alipohamia ACT-Wazalendo na kuondoka na kundi kubwa la wanachama.

“Lakini ni Maalim huyo ambaye amechangia kutuliza hali ya hewa Zanzibar, ingawa baadhi ya watu walimwona kama msaliti pale alipokubali kushiriki kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa,” anasema.

Anafafanua kuwa Wazanzibari walimwona Maalim Seif kama taasisi hadi kufikia kusema kuwa CUF ni Seif na Seif ni CUF, kwa kuwa walimuona ndiye anayefaa kuwaongoza.

Mwanasiasa huyo anasema, kwa mtazamo huo, alisababisha watu wa wamfuate yeye badala ya itikadi ya chama, na kwamba mazingira hayo yanaweza kuchangia upinzani kukosa nguvu Zanzibar.

“Pamoja na mengi aliofanya ikiwamo kusaidia kuwanganisha Wazanzibar, mimi ninaona kosa la kiufundi alilotebda la kutoandaa watu wa kuvaa viatu vyake ili upinzani uendelee kuwa na nguvu,” anasema.





# Wataalamu maendeleo jamii kuteta

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

CHAMA cha Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (CODEPATA), leo kinatarajia kufanya kongamano kujadili masuala mbalimbali zikiwamo kero zinazowakabili ili kada iwe na tija.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Rais wa chama hicho, Wambura Sunday, alisema kongamano hilo litakutanisha wataalamu takribani 400.

Alisema kongamano hilo ni muhimu kwa sababu litawakutanisha wataalamu wa maendeleo ya jamii kutoka maeneo mbalimbali ili kubadilishana uzoefu, mbinu na mikakati itakayosaidia kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

"Tutakutanisha wanachama ili kupeana mbinu na mikakati itakayowezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufasaha zaidi pia kubadilishana uzoefu na mbinu mpya," alisema Wambura.

Alisema pamoja na mada mbalimbali zitakazowasilishwa, pia kutakuwa na maonyesho ya bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa na vikundi vya wajasiriamali, watu binafsi, asasi za kiraia na taasisi.

"Tutawasilisha mada mbalimbali na majadiliano zitawasilishwa na kujadiliwa wakati wa kongamano kati ya mada sita, tatu zitawasilishwa katika majadiliano ya vikundi," alisema.

"Pia tutazindua tovuti ya chama, uchaguzi mkuu wa chama kuchagua rais, makamu wa rais, katibu wa chama, mweka hazina na waratibu wa kanda saba," aliongeza.

Alisema Katibu Mkuu Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jongu, atawasilisha mada kuu kuhusu uongozi wa kimkakati katika kutekeleza na kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii.

Alisema mkutano huo ni wa nne na mikutano mitatu imeshafanyika wakishirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tangu mwaka 2017 ikishirikisha sekretarieti za mkoa, mamlaka za serikali za mitaa, taasisi za wizara, na wizara za kisekta na asasi za kiraia.

Wambura alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali za maendeleo ya kijamii, lakini bado hazijatambuliwa na jamii.

Katibu Mkuu wa CODEPATA, Paschal Mahinyila, alisema chama hicho kilianzishwa rasmi mwaka 2017 na kusajiliwa rasmi mwaka 2019 sambamba na kuweka miongozo mbalimbali katika kuendesha taaluma hiyo.

Naye Mratibu wa CODEPATA, Kanda ya Ziwa ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa chama hicho, Aliadina Peter, alisema walianzisha chama hicho kwa lengo la kusimamia taaluma hiyo ili kufanya kazi vizuri katika taaluma ya maendeleo ya jamii.

# RC Mahenge ataka tathmini sera, matamko vifo vya mama na mtoto

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza kufanyika kwa tathmini juu ya sera na matamko yanayohusu udhibiti wa vifo vya mama na mtoto, ili kujua kama yanasaidia katika udhibiti hali hiyo nchini.

Dk. Mahenge alitoa ushauri huo jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha kujadili mpango mkakati wa kupunguza vifo vya mama na mtoto Kanda ya Kati.

Alisema mara nyingi kumekuwa na matamko mengi na sera juu ya udhibiti wa vifo vya mama na mtoto ni wakati kufanya tathmini ili kuona ufanisi wake.

"Tuna matamko mengi na sera je, zimetufikisha wapi? Nashauri mkae mwangalie tumefanikiwa wapi na tumekwama wapi ili turekebishe na kupunguza hivi vifo vya mama na mtoto ambavyo vingi vinaepukika," alisema.

Hata hivyo, alisema takwimu zinaonyesha vifo vya uzazi vinaongezeka licha ya mikakati iliyofanyika kwa kanda ya kati, ambapo 2019 kulikuwa na vifo 162 na mwaka 2020 kuna vifo 175.

Alitaja baadhi ya vitu vinavyochangia vifo hivyo ni kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua kwa kinamama, kifafa cha mimba, kupasuka kwa mji wa uzazi na uambukizo mkali, ambavyo vinazuilika kupunguza vifo vya uzazi.

"Vifo vya watoto wachanga pia ni tatizo katika kanda hii takwimu zinaonyesha kupungua ambapo mwaka 2019 kulikuwa na vifo 1,173 na mwaka 2020 kulikuwa na vifo 1,009," alisema.

Dk. Mahenge alitaja vitu vinavyosababisha vifo kwa watoto ni kushindwa kupumua baada ya kuzaliwa, mtoto kuzaliwa kabla ya wakati na mtoto kuzaliwa na uzito pungufu na pneumonia.

Mkurugenzi wa Huduma ya Kinga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alisema mpaka sasa wamepiga hatua kubwa katika mapambano ya kuzuia vifo vya mama na mtoto kwa kuimarisha huduma za msingi za afya.

Alisema katika kikao hicho watatumia katika kutathmini utekelezaji wa mpango wa mapambano dhidi ya kupunguza vifo vya uzazi hasa kwa mama na mtoto na kuweka mikakati mipya kuhakikisha wanapunguza vifo vya uzazi na kupokea utekelezaji wa mpango huo kwa halmashauri.

Dk. Subi alibainisha kuwa wizara imejiwekea malengo kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 vifo vya uzazi vinapungua hadi kufika vifo chini ya 70 kati ya vizazi na 100,000 katika kuhakikisha tatizo hilo linapungua na kuwa na takwimu sahihi, amewataka wakurugenzi kupata takwimu za vifo vya uzazi kila siku asubuhi wakishirikiana na watendaji wa ngazi zote katika halmashauri zao.



Mfanyabiashara wa malimao, Tawakali Ngasso, akiyapanga katika soko kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, ambapo bidhaa hiyo, imekuwa na mahitaji makubwa kwa hivi sasa, baada ya wataalamu wa afya kushauri kutumia kwa wingi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jiji lakomaa na vifungashio vya nje

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, Jemes Yuna, amewataka wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa za matunda na nyanya kwenye vifungashio kuondoka navyo pindi wanapomaliza kushusha ndani ya masoko.

Yuna alisema hayo jana alipokuwa akitoa elimu kwa wafanyabiashara ambao wanaosafirisha bidhaa zao zikiwa kwenye vifungashio na kushusha katika masoko yaliyoko ndani ya Jiji la Dodoma.

Alisema bado kuna wafanyabiashara wanaoshusha bidhaa zao zikiwa katika vifungashio kutoka nje ya mkoa na kuvitelekeza kwenye masoko, hatua ambayo ni kinyume kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizoko ndani ya halmashauri.

Ofisa huyo alisema bidhaa hizo zinazoletwa zikiwa kwenye vifungashio, hivyo vinatakiwa kukusanywa na kuondolewa kwa kuwa taka zinazotakiwa kubaki ni zile zinazozalishwa na wafanyabiashara ndani ya masoko.

"Suala la usafi ni la kila mmoja wetu, awe mfanyabiashara wa kutoka nje ya mkoa au wa ndani vinginevyo wote wanatakiwa kujiweka kwenye mazingira ya usafi, na hususani kwenye maeneo ambayo yanayotumika kwa shughuli za kujiingizia kipato," alisema.

Alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaotumia magari kusafirisha bidhaa kama vile matunda na nyanya zikiwa kwenye vifungashio na wakishashusha huziacha bila kuziondoa.

Ofisa huyo aliwataka wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, kuhakikisha kwenye maeneo yao wanayofanya shughuli za kibiashara, kuhakikisha wanadhibiti uchafu kwa kuweka takataka katika mazingira yaliyo rafiki kwa ajili ya kuziondoa.

Alisema wengi wamekuwa wakifanya biashara zao na kuziacha takataka bila kuzidhibiti na kusababisha kuzagaa ovyo mitaani, hali ambayo imekuwa ikileta sura mbaya ndani ya jiji.

Makamu Mwenyekiti wa Machinga Mkoa wa Dodoma, Bruno Mponzi, aliwataka machinga kuhakikisha wanatoa ushirikiano mkubwa katika usafi wa mazingira kwenye mitaa mbalimbali ambayo wanayofanyia biashara na kujiingizia kipato.

Alisema badala ya kusubiri takataka hizo kuondolewa na wengine, wanatakiwa kuwa mabalozi wa mfano wa kuziondoa ili kuunga mkono juhudi kubwa zinazofanywa na jiji katika kuhakikisha usafi wa mazingira unadumu siku zote.





# Takwimu za vifo vya uzazi tishio

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TAKWIMU za vifo vitokanavyo na uzazi nchini, zinatisha ambapo kuanzia mwaka 2018 mpaka sasa wanawake kati ya 1,700 na 1,800 hupoteza maisha kila mwaka wakati wa kujifungua kutokana na sababu mbalimbali.

Mkurugenzi Msaidizi Afya ya Uzazi na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Ahmad Makuhani, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa kikao cha kujadili namna ya kukabiliana na vifo hivyo, kilichohusisha wataalamu kutoka mikoa ya Mbeya, Rukwa na Songwe.

Alisema mbali na vifo hivyo vya kinamama, pia watoto wachanga kati ya 10,000 na 12,000 hufariki kila mwaka nchini, hali ambayo inahitaji ushirikiano wa wadau katika kukabiliana na matatizo hayo.

Dk. Makuhani alisema asilimia 90 ya vifo hivyo hutokea katika vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na makundi hayo kukosa huduma sahihi ambazo yanastahili kutokana na hali zao pamoja na kukosekana kwa stadi sahihi miongoni mwa watoa huduma. "Hali hii haikubaliki, hawa ni Watanzania ambao tulikuwa tunatarajia kwamba wangeweza kuchangia katika maendeleo ya nchi hii, sasa lazima tujiulize kwamba tumefanikiwa wapi na tumeshindwa wapi turekebishe," alisema Dk. Makuhani.

Aidha, Dk. Makuhani alisema pamoja na matatizo hayo ya vifo vya mama na mtoto kumekuwa na ongezeko la utumiaji wa huduma za afya ikiwamo mahudhurio ya wajawazito kliniki kufuatilia maendeleo ya ujauzito wao.

Alisema kwa sasa mahudhurio ya wajawazito mara nne yameongezeka na kufikia zaidi ya asilimia 75, wanawake wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wamefikia zaidi ya asilimia 80 na kinamama wanaoenda kliniki saa 48 baada ya kujifungua imefikia zaidi ya asilimia 70.

Alisema ili kukabiliana na matatizo hayo yanayosababisha vifo, wadau wanatakiwa kuimarisha uongozi na usimamizi ili kutia chachu katika kupunguza vifo.

Akizungumza huku akichanganya na mizaha, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kwa kawaida madaktari huwa hawazuii vifo bali huwa wanachelewesha vifo kwa maelezo kuwa kifo kipo wakati wote.

Chalamila alisema wakati mwingine vifo hivyo vya kinamama na watoto huwa vinatokea kwa sababu ya matatizo ya uongozi kwenye maeneo husika, hivyo akawataka wahusika kuimarisha uongozi wao kwenye maeneo wanayoongoza.

Alisema mikakati ambayo wataalamu wanaanzisha inaweza ikasaidia kuchelewesha vifo vya mama na mtoto endapo wataimarisha stadi za uongozi.

"Pamoja na takwimu hizo kuonyesha kwamba vifo vya mama na mtoto viko juu, lakini ni ukweli usiopingika kwamba idadi ya vifo imepungua ukilinganisha na miaka ya nyuma, takwimu za mwaka 2016 hazilingani na za 2020," alisema Chalamila.

Aliwataka Watanzania kuwa na utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili wakibainika kuwa na maradhi watibiwe haraka, huku akiwataka kuacha hofu isiyokuwa na sababu ikiwamo ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-UWSA), wakiendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji katika mradi wa maji wa Mwashali-Isyesye jana, ambao unatarajiwa kukamilika Februari 28, mwaka huu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watendaji wabanwa matumizi ya fedha

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, limeiagiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, kuwachukulia hatua watendaji wote wanaokusanya mapato na kuzitumia fedha kwa shughuli ambazo hazijaidhinishwa.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mpokigwa Mwankunga, alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha baraza hilo cha kawaida, ambapo alisema kumekuwa na tabia ya watendaji hao kufuja fedha za serikali kwa kutumia mapato ghafi.

Alisema kwa mujibu wa sheria, kila fedha inayokusanywa inatakiwa ionekane kwenye akaunti za halmashauri kisha kutumika kwa kazi ambazo zimeidhinishwa na serikali.

"Nakuagiza mkurugenzi wale wote ambao wameonekana kuanza kuzitumia fedha hizi kinyume cha malengo, anza kuwachukulia hatua ili wazirejeshe haraka sana ili zifanye kazi zinazotakiwa," alisema Mwankunga.

Aidha, alisema halmashauri hiyo imefanya vizuri kwenye ukusanyaji wa mapato katika kipindi hiki ambapo mpaka sasa imefikia asilimia 56, na kwamba kwa mwendo huo mpaka kufikia Julai watakuwa wamefikia zaidi ya asilimia 100.

Alisema ili kufikia kiwango hicho kila mtendaji anatakiwa kushiriki kikamilifu kwenye kukusanya mapato hayo na kuyawasilisha halmashauri.

Alisema mwaka huu halmashauri hiyo ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 25 kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza, na kwamba mpaka sasa vyumba hivyo vimekamilika na wanafunzi wote wameshaanza masomo.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Eliah Chigoji, alisema Tume ya Mkoa iliyokuwa imeundwa kufuatilia ukusanyaji wa mapato ilibaini kuwa asilimia kubwa ya wenye dhamana ya kukusanya mapato sio waaminifu.

Aliwataka ambao wanakusanya fedha hizo kuhakikisha wanaziwasilisha halmashauri ili kuepuka madeni ambayo hayana ulazima na kwamba kutumia fedha za serikali bila idhini ni kosa kwa mujibu wa sheria.

"Mtu unakusanyaje fedha za serikali halafu unakaa nazo? Kuna watu inaonyesha wanadaiwa sasa naomba madeni hayo ni halali si walipe? Sasa naomba wafuatiliwe ili walipe," alisema Chigonji.

Alisisitiza watendaji wa serikali kujiepusha na matumizi mabaya ya fedha za serikali ili kuepuka adhabu ambazo zinaweza zikawakumba ikiwamo kufukuzwa kazi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Castory Makeula, aliwataka watendaji wa kata na vijiji kuwasilisha mapato hayo benki kwa wakati ili kuepuka mkono wa sheria.

Alisema wanaendelea kuwabana watendaji ambao wanadaiwa fedha za halmashauri hizo ili wazirejeshe na ziingizwe kwenye matumizi yaliyoidhinishwa na Baraza la Madiwani.

Alisema wanaendelea kushirikiana na baadhi ya vyombo ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwabana watendaji ambao hawawasilishi makusanyo ili wazirejeshe.

# Mchimbaji dhahabu ajitolea ujenzi shule

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

MCHIMBAJI wa dhahabu katika Mji wa Makongolosi wilayani Chunya, George Mtasha, amejitolea kujenga shule ya msingi katika Mji huo, ili kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye shule chache zilizopo kwenye mji huo.

Akizungumza jana na Nipashe, Mtasha ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wilaya ya Chunya alisema mpaka sasa ametumia zaidi ya Sh. milioni 40 kujenga shule hiyo na anaendelea na ujenzi huo.

Alisema aliamua kujitolea baada ya kubaini kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi kwenye shule zilizopo kwenye mji huo hali ambayo imesababisha kuwapo na msongamano wa wanafunzi hao.

Alisema katika mji huo zipo shule za msingi za serikali nne pekee ambazo ni Shule ya Msingi Makongolosi, Chipoka, Nyerere na Kilombero na kwamba shule anayoijenga itakuwa ya tano na itasaidia kupunguza msongamano kwenye shule za zamani.

"Nimeamua kujitolea kujenga shule hii kama mchango wangu kwenye maendeleo ya wananchi wa mji huu ambao mimi nimewekeza shughuli zangu, lakini ni sehemu ya kuiunga mkono serikali kwenye uboreshaji wa sekta ya elimu nchini," alisema Mtasha.

Hata hivyo alisema anapata ushirikiano mzuri kutoka serikalini kutokana na kupeleka wataalamu mara kwa mara kukagua ujenzi huo na pamoja na kushauri namna bora ya miundombinu hiyo kuwa.

Alisema mradi huo ni historia anayotaka kuiweka katika mji huo ili kuwasaidia watoto wa mji huo kupata elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao.

Alisema baada ya kuikamilisha shule hiyo ataikabidhi kwenye uongozi wa Halmashauri ya Mji huo kwa ajili ya kuendelea na taratibu za usajili pamoja na kuifungua.



# Mkuya akoleza moto sakata la vileo

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa zamani wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Saada Mkuya, amesema Bodi ya Vileo Zanzibar imevunja sheria na Katiba kwa kuruhusu kampuni sita kuingiza pombe badala ya tatu.

Pia amesema kuna ukiukaji wa sheria namba 9 ya mwaka 2020, jambo ambalo amesema waliotekeleza wamekwenda kinyume cha matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mkuya alitoa matamshi hayo wakati akichangia hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Sh. trilioni 1.5 katika mkutano wa pili wa Baraza la Wawakilishi unaoendelea.

Mkuya alisema Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kudhibiti na Kusimamia Uingizaji, Uhifadhi Uuzaji, Usambazaji na Unywaji Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020, imeweka ukomo kwa kampuni tatu tu ndizo zinazotakiwa kupewa vibali vya uingizaji vileo Zanzibar.

Alisema kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Baraza la Wawakilishi ndilo lenye dhamana ya kutunga sheria, na kwamba Bodi ya Vileo imefanya makosa kutoa vibali zaidi ya vitatu, jambo ambalo alisema ni kinyume cha sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika baada ya Rais wa Zanzibar kusaini Mei, mwaka 2020.

"Sheria inataja kibali cha kuingiza kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu, leo waingizaji vileo wamefikia sita Zanzibar," alisema Mkuya, huku wajumbe wakimsikiliza kwa makini.

"Leo tunasikia watendaji wanasema wametumia busara eti kwa sababu serikali inahitaji kukusanya mapato. Kufikia waingizaji sita ni kuvunja sheria inawataja watatu, huko ni kwenda kinyume cha utashi wa kikatiba," Mkuya.

Alisema kimsingi, lengo la baraza la kutunga sheria mpya ya vileo limevunjwa na Bodi ya Udhibiti na Kusimamia Vileo Zanzibar, jambo ambalo halikubaliki katika kufuata misingi ya utawala wa sheria.

"Leo wanakuja watendaji wanasema sisi tumetumia busara kuongeza waingizaji kwa sababu serikali inahitaji mapato. Nani aliyewaambia serikali kama inahitaji kukusanya mapato iende kinyume cha sheria na kuvunja katiba?" Alihoji Mkuya. Mkuya alisema kumekuwapo na ongezeko la baa Zanzibar na kutoa mfano katika Mtaa wa Mbweni kilomita moja kuna baa zaidi ya tisa katika mtaa huo, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Mpaka sasa Wawakilishi waliojitokeza kuzungumzia uvunjwaji wa sheria uliyofanywa na Bodi ya Udhibiti na Usimamisi wa Vileo ni Mwakilishi wa Viti Maalum, Salha Mwinyijuma Mohamed ambaye alisema bodi haina mamlaka ya kisheria kuweka kando sheria na kutoa vibali kwa kampuni kuingiza vileo kinyume cha sheria.

Alisema kama sheria ilikuwa na kasoro katika utekelezaji wake, walitakiwa kushauri serikali ipeleke mapendekezo ya marekebisho ya sheria badala ya kufanya maamuzi yanayokwenda kinyume cha sheria.

Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulratifu, alisema inasikitisha sheria ya vileo imeanza kuvunjwa miezi 10 tangu kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika Januari mwaka huu.

Alisema kampuni zote zilizopewa vibali vya ziada vya kuingiza vileo Zanzibar zitakuwa zinafanya biashara kinyume cha sheria ya vileo namba 9 ya mwaka 2020.

Lakini Mwenyekiti wa Bodi ya Vileo Zanzibar, Bwana Abdulrazaki Abdulkadiri, alisema wamelazimika kutoa vibali hivyo kwa kampuni zaidi ya tatu za kuingiza vileo kinyume cha sheria, ili kulinda mapato ya serikali kupitia kodi na tozo za vibali.

Wakati hayo yakiendelea kujitokeza, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), Sheikh Khamis Yussuf Khamis, alisema wameamua kufungua kesi Makahama Kuu dhidi ya bodi baada ya kuvunja sheria kwa kutoa vibali kwa kampuni nane badala ya tatu kinyume cha sheria.

Aidha, alisema kwa mujibu wa kifungu cha 28(k) sheria ya vileo kimesema baa kabla ya kuanzishwa lazima iwe umbali wa mita 1,000 kutoka katika eneo la huduma za jamii kama shule, hospitali, madrasa au nyumba ya ibada, lakini masharti ya sheria yamekuwa yakipuuzwa na bodi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisaini kitabu cha maombolezo ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Mji Mkongwe kupandishwa hadhi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inakusudia kuupandisha hadhi Mji Mkongwe wa Zanzibar na kuufanya kuwa sehemu ya kivutio cha watalii kwa kutumia majengo ya kale na makumbusho ya kihistoria.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, wakati akielezea mikakati ya wizara katika kukuza sekta ya utalii na vivutio vyake. Alisema Mji Mkongwe umebeba historia kubwa ya mambo ya kale kwa kutumia tawala mbalimbali zilizopata kuongoza Zanzibar zikiwamo Waarabu na Wareno.

Aliyataja maeneo ambayo yatatumika kwa ajili ya kuutangaza Mji Mkongwe wa Zanzibar ni Kanisa la Mkunazini ambalo mchango wake katika kutokomeza biashara ya utumwa ni mkubwa.

Aidha, aliyataja maeneo ya jengo la wananchi la Forodhani ambalo yapo makaburi ya watawala wote waliotawala Zanzibar kabla ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964.

"Mji Mkongwe wa Zanzibar tutaugeuza kuwa kitovu cha utalii Zanzibar kutokana na hadhi yake ya kuwa na vivutio vingi vyenye historia ya mambo ya kale," alisema.

Mji Mkongwe wa Zanzibar umeingizwa na kutambuliwa kuwa na hadhi ya urithi wa kimataifa, kutokana na kutunza majengo ya kihistoria ya mambo ya kale yaliyopo hadi leo.

**"Mji Mkongwe wa Zanzibar tutaugeuza kuwa kitovu cha utalii Zanzibar kutokana na hadhi yake ya kuwa na vivutio vingi vyenye historia ya mambo ya kale," alisema.**

# Deni la Zanzibar lafikia bil. 896/-

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, amesema deni la taifa limefikia Sh. bilioni 896.2 likiwa lipo chini ya asilimia 22 ambalo ni himilivu na linairuhusu Zanzibar kukopa katika miradi yenye tija ya kukuza uchumi na maendeleo.

Ali alisema hayo wakati akijibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2021-2024 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema deni la nje limefikia Sh. bilioni 691.5 ambapo asilimia 95.9 linadhaminiwa na kulipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo miradi mikubwa ya majisafi na salama, huku asilimia 4.1 lipo chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, alisema deni la ndani limefikia Sh. bilioni 204.9, ambalo kutoka katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Zanzibar (ZSSF) ni Sh. bilioni 51.7 na hatifungani kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ni Sh. bilioni 154.1.

Alisema hadi kufikia Desemba mwaka 2020, wastani wa uwiano wa deni la taifa kwa uchumi ni asilimia 22 ikiwa ni chini ya kiwango cha ukomo kinachokubalika kimataifa cha asilimia 50.

Alisema kiwango hicho kinaashiria kwamba hali ya deni ni himilivu na Zanzibar inao uwezo wa kukopa fedha kwa ajili ya miradi ya kimkakati zaidi yenye tija katika kukuza uchumi wake.

"Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha uwiano wa deni la taifa kwa uchumi kimefikia asilimia 22...kiwango hicho kinaashiria kwamba deni letu ni himilivu na tunaweza kukopa zaidi katika miradi yenye tija ya kimkakati kukuza uchumi," alisema.

Waziri huyo alisema kwamba serikali itakopa fedha katika miradi muhimu kwa kuzishirikisha sekta binafsi ikiwamo ujenzi wa bandari na sekta ya uwekezaji wa uchumi wa bluu na nishati ya umeme.

Alisema miradi ya uchumi wa bluu ndiyo kipaumbele cha serikali katika kufikia malengo yake ya kuona Zanzibar inafikia uchumi na kuwa kitovu cha biashara katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati.

"Tumejikita katika uwekezaji wa uchumi wa bluu kwa kushirikiana na sekta binafsi, ambazo tumezipa nafasi ya kushirikiano nazo kuona tunapiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi," aliongeza.

HABARI KIMATAIFA

# Wakenya kupigia kura marekebisho Katiba mpya

**Nairobi, KENYA**

KENYA inatarajiwa kuandaa kura ya maamuzi kuhusu marekebisho ya Katiba, baada ya muswada wa Building Bridges Initiative (BBI), kuidhinishwa katika mabunge 24.

Mabunge ya majimbo 10 zaidi yanajadili muswada huo kwa sasa, huenda idadi ya majimbo yanayounga mkono mchakato huo kuongezeka.

Ijapokuwa muswada wa BBI utahitajika kuidhinishwa na Bunge la Kitaifa na Bunge la Seneti, kura ya maamuzi itafanyika hata mabunge hayo yasipouunga mkono.

Baadaye maspika wa mabunge hayo mawili watamfahamisha rais kuhusu uamuzi wao.


BBI, ni Jopokazi la Maridhiano nchini Kenya handshake, lilianzishwa Machi 9, mwaka 2018, baada ya Rais Uhuru Kenyatta na mpinzani wake mkuu wa kisiasa, Raila Odinga kuamua kusalimiana hadharani.

Hatua hiyo ilimaliza wasiwasi wa miezi kadhaa kufuatia uchaguzi uliokumbwa na utata, ambao mara kwa mara husababisha migawanyiko na kusababisha ghasia nchini Kenya.

Kwa upande mmoja, kwa sababu matokeo ya uchaguzi yalikuwa yamefutwa na mahakama ya juu nchini Kenya na uchaguzi ulirudiwa na kususiwa na Raila Odinga.

Lengo kuu la BBI likiwa kuunganisha taifa ambalo nusura litumbukie kwenye vita kufuatia uhasama uliozuka baada ya kinyang'anyiro cha uchaguzi wa urais, mwaka wa 2017.

Viongozi hao walikubaliana kuunda kamati iliyolenga njia ya kumaliza hali hiyo ya ukosefu wa uthabiti.



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta (kushoto) na Kiongozi wa Upinzani, Raila Odinga. Viongozi hawa waliunda kamati ya watu 14 na mikutano ya umma kwenye majimbo 47, ili kupokea maoni baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2017. **PICHA/MAKTABA**

## Maelfu waathiriwa na mafuriko Indonesia

**Jakarta, INDONESIA**

WATU 28,000 wameathiriwa na mafuriko katika eneo la Bekasi na Karawang katika Jimbo la Java Magharibi.

Mafuriko yalitokea katika eneo la Bekasi na Karawang katika Jimbo la Java Magharibi mwa Indonesia.

Raditya Jati, Mkuu wa Kituo cha Habari na Mawasiliano cha Wakala wa Kitaifa cha Maafa, alisema katika taarifa kwamba vijiji vinne vya Bekasi na vijiji 34 vya Karawang viliathiriwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa tangu wikiendi.

Ripoti ilisema kwamba kiwango cha maji kimeongezeka hadi mita 2.5 katika baadhi ya mikoa, Jati amesema kuwa zaidi ya watu elfu 28 waliathiriwa na mafuriko, na kwamba uhamishaji wa watu 4,184 kwenda maeneo salama unaendelea.

***TRT***

## Theluji yaleta hofu wakimbizi Lebanon

**Beirut, LEBANON**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), limesema hali mbaya ya hewa inayoambatana na baridi kali na theluji Mashariki ya Kati, imeongeza wasiwasi kwa mamilioni ya wakimbizi.

Nchini Lebanon katika makazi yasiyo rasmi ya wakimbizi bonde la Beka, theluji imesababisha athari kwa asilimia 70 ya makazi.

UNHCR ilisema maelfu ya wakimbizi wameathirika na kiasi kikubwa tangu Februari 12, mwaka huu, nchini Lebanon na kusababisha baridi kali, mvua kubwa, barafu na upepo mkali.

Mahema mengi katika makazi ya bonde la Beka yamejengwa kwa maturubahi yanavuja na kuzidiwa uzito na theluji na kuporomoka.

Shirika hilo lilisema hofu ni kwa ambao hawana huduma muhimu, ikiwamo majiko ya kupasha joto mahema yao.

Mamlaka ya Lebanon na wadau wengine wa misaada UNHCR, wameanza kupeleka msaada wa dharura ikiwamo mavazi ya baridi, vifaa vya kupasha moto mahema, ukarabati wa mahema.

***UN***

## Rais Biden aomboleza vifo 500,000 corona

**Washington, MAREKANI**

RAIS Joe Biden ametoa wito kwa taifa kuungana nae katika kuwakumbuka waliopoteza wapendwa wao kutokana na virusi vya COVID-19.

Juzi jioni alitembea upande wa pili wa jengo la White House, uliopambwa kwa bendera nyeusi pamoja na mishumaa 500, ikiwa ishara kuomboleza vifo laki tano sababu ya COVID-19.

Rais Biden alikuwapo na mkewe Jill Biden na Makamu Rais Kamala Harris pamoja na mumewe Doug Emhoff.

Wote walisimama kimya wakati bendi ya Marine Corps ikipiga wimbo wa Amazing Grace.

Dakika chache kabla, ukumbi wa Cross Hall ghorofa ya kwanza ya White House, Rais Biden alitoa wito kwa taifa kuungana nae katika ukimya kukumbuka wapendwa wao kutokana na virusi vya COVID-19.

***VOA***

# Waasi FDLR-FOCA wahusishwa mauaji balozi

**Goma, DRC**

SIKU mbili tangu kifo cha Balozi wa Italia nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Luca Attanasio, kundi la waasi wa FDLR-FOCA, wenye asili ya Rwanda, limetajwa kuhusika.

Balozi Attanasio alishambuliwa na kuuawa juzi karibu na mji wa Goma, Mashariki mwa DRC.

Balozi alikuwa katika msafara wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na gari lao kushambuliwa.

Hata hivyo, kundi la FDLR -FOCA, limekanusha kuhusika na shambulizi hilo, na kwamba vikosi vyake viko mbali na eneo la shambulizi hilo.

Maofisa katika mbuga ya wanyamapori ya Virunga walisema, shambulio hilo lilikuwa jaribio la utekaji nyara lililoshindikana.

Makundi mengi ya wapiganaji wenye silaha yameendelea kujiimarisha ndani na pembezoni mwa mbuga hiyo, inayopakana na nchi jirani za Rwanda na Uganda.

Waziri wa Mambo ya Nje wa DRC, Marie Ntumba Nzeza alisema kuwa, serikali imeanza uchunguzi kubaini wahusika wa mauaji hayo na kwamba bado hawajakamatwa.

Mbali na balozi huyo wa Italia kuuawa, ofisa wa ubalozi wa Italia, dereva wa gari raia wa Congo pia waliuawa katika tukio hilo. Kwa mujibu wa WFP abiria wengine waliokuwa wakisafiri na ujumbe huo wamejeruhiwa wakati wa shambulio hilo.

Ujumbe huo ulikuwa unasafiri kutoka Goma kuzuru programu ya WFP ya mlo shuleni katika eneo la Rutshuru wakati shambulio hilo lilipotokea.

***RFI/UN***



# KLOPP

## AKATA TAMAA YA UBINGWA EPL

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesema kwa mwendo ambao Liverpool wanakwenda nao kwa sasa anaamini itakuwa ngumu kwao kutetea taji la Ligi Kuu England, EPL.

Liverpool inapitia kwenye kipindi kigumu kwa sasa ndani ya uwanja kwa kuwa haipati matokeo chanya, jambo linalompasua kichwa kocha huyo ambaye ni bingwa mtetezi.

Juzi ilikubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa majirani zao Everton kwenye uwanja wa Anfield na kuwafanya wabakie kwenye nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Liverpool imecheza mechi 25 za Ligi Kuu England na imekusanya pointi 40 kibindoni kwa msimu wa 2020/21.

Klopp akizungumza na waandishi wa habari amesema: "Ligi ni ngumu na kila timu inahitaji kufanya vizuri, hivyo ninaona kwamba kuna ugumu kwenye kutetea taji la ligi licha ya kwamba lolote linaweza kutokea.

"Kwa mwenendo wa Liverpool kwa sasa, nafasi ya kulitetea taji hili ni ngumu sana, ingawa kwenye mpira wa miguu lolote linaweza kutokea," alisema Klopp.

Matokeo mabovu inayopata ni kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wachezaji ambao wanasumbuliwa na majeraha ikiwa ni pamoja na beki kisiki, Virgil Dijk na Fabinho.

# Arteta ajipanga kumbakiza Odegaard

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anafanya kila jitihada kuhakikisha, Martin Odegaard anasalia klabuni hapo hata baada ya kumalizika kipindi chake cha mkopo.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, Arsenal wanataka kumbakiza nyota huyo ambaye anacheza kwa mkopo akitokea Real Madrid.

Madrid wenyewe wameshabainisha kwamba, watamhitaji mchezaji huyo mwishoni mwa msimu wakati ambao atakuwa amemaliza kipindi chake cha kucheza kwa mkopo.

Hata hivyo, Arteta amebainisha baada ya msimu huu, watakaa mezani ili kujadili na kuamua hatima ya uhamisho wa nyota huyu.

"Mwisho wa msimu huu tunatarajia kukaa chini na kuangalia kama tunaweza kuendelea zaidi kuwa na Martin, ni jambo ambalo halitegemei upande wetu pekee," alisema Arteta akinukuliwa na Sky Sport.

Odegaard anatajwa kutokuwa na uhusiano mzuri sana na Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, na upande wa Real Madrid bado hawana uhakika na kile ambacho wanataka kukifanya juu ya nyota huyo.

Uzuri ni kwamba, Odegaard mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kuendelea kucheza kwenye dimba hilo la Emirates baada ya kipindi chake cha mkopo kumalizika.



# Rodgers atajwa kumrithi Mourinho

**LONDON, England**

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers ameripotiwa kuwa anaongoza kwa makocha wanaopewa nafasi ya kuchukua mikoba ya Jose Mourinho katika kikosi cha Tottenham Hotspur.

Mustakabali wa Mourinho kwenye klabu hiyo yenye maskani yake London Kaskazini umekuwa na walakini na ni suala linalopewa mjadala mkubwa kutokana na hali ya hivi karibuni kufanya vibaya kwenye Ligi Kuu England, ambapo wamepoteza mechi nne kati ya tano za mwisho.

Mourinho raia wa Ureno, anaonekana kuwa mbioni kupoteza kibarua chake kama msimamizi wa timu hiyo, kama vile ilivyo kwa Jurgen Klopp kule Liverpool, ingawa mwenyekiti wa klabu ya Spurs, Daniel Levy ameripotiwa tayari kumpa muda wa kufanya mabadiliko hapo Tottenham.

Hata hivyo, kwa mujibu wa chanzo kimoja cha ndani ya Spurs, Levy alitaka Rodgers kuchukua nafasi klabuni hapo mwaka 2012, kabla ya kuchukua kazi ya Liverpool, na raia huyu wa Ireland Kaskazini atakuwa kipaumbele kwa bosi huyo endapo Mourinho atatumbuliwa.

Rodgers amefanya kazi nzuri kule Leicester msimu huu, wakiwa wanashika nafasi ya tatu katika jedwali la Ligi Kuu England.

Kocha wa klabu ya RB Leipzig ya nchini Ujerumani, Julian Nagelsmann - ambaye hapo awali alikuwa akihusishwa na Chelsea, pia ametajwa kama mbadala wa Mourinho.



HABARI MICHEZO



## LIVERPOOL YAJIPANGA KUMSAJILI OCAMPOS

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL inahusishwa na mpango wa dili la mabadilishano ya kumnasa nyota wa Atletico Madrid, Lucas Ocampos ili atue Anfield katika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Kocha Jurgen Klopp anatajwa anamfuatilia kwa ukaribu nyota huyo raia wa Argentina katika mpango wake wa kuboresha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Kwa mujibu wa La Razon, Klopp yupo tayari kufanya mabadilishano na kuongeza kiasi cha fedha kitakachotakiwa.

Dili la mabadilishano litamhusisha mchezaji wao, Takumi Minamino raia wa Japan kwenda Atletico ambao wanatumia Uwanja wa Ramon Sanchez Pizjuan.

Minamino kwa sasa anacheza kwa mkopo Southampton baada ya kukosa nafasi katika kikosi chake kwanza cha Anfield.

Wachezaji hawa wawili wanatofautiana thamani na Ocampos mkataba wake una thamani ya pauni milioni 56, wakati Minamino akiwa na thamani ya pauni milioni 10 na Liverpool wapo tayari kulipa kiasi kitakachotakiwa.

## UNITED YAJIIMARISHA KUMNASA ANSU FATI

**MANCHESTER, England**

IMEELEZWA Klabu ya Manchester United imemtengea pauni milioni 130 nyota wa Barcelona, Ansu Fati ili kupata saini yake baada ya dili lake msimu uliopita kutua Old Trafford kukwama.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 18 yupo kwenye kikosi cha kwanza kwa sasa na anauwezo mkubwa wa kucheka na nyavu jambo ambalo linawapa nguvu United kuipambania saini yake.

Akiwa ndani ya Nou Camp tangu msimu uliopita amefunga jumla ya mabao nane kwenye mechi 33 ambazo alipata nafasi ya kucheza.

Ofa ya mwanzo ndani ya Barcelona ilikataliwa na rais aliyejiuzulu, Josep Bartomeu kwa kile alichoeleza hawawezi kuacha kipaji hicho kiondoke, ingawa kwa sasa anapewa nafasi kubwa ya kuondoka ndani ya La Liga na kuibukia kwenye Ligi Kuu England kutokana na timu hiyo kuyumba kiuchumi.

Hata hivyo, Fati kwa sasa anauguza majeraha na anatarajia kurudi uwanjani katikati ya Aprili mwaka huu.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solkjaer baada ya kumkosa Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund, anaona kwamba Fati ndiye mwenye nafasi kubwa ya kutua hapo Old Trafford.

# HAALAND

## NI MASHINE YA MABAO - REUS

**DORTMUND, Ujrumani**

MARCO Reus amempa sifa mchezaji mwenzake wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kwa kumwita 'mashine' ya mabao.

Haaland baada ya kufunga mabao mawili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akafunga tena kwenye mchezo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, dhidi ya Schalke.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alifunika kwenye vichwa vya habari siku ya Jumatano kufuatia ushindi wake mzuri wa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Sevilla.

"Erling ni mashine kamili," alisema Reus akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Ana njaa sana ya mabao. Unaliona hilo katika kila mchezo. Tunatumaini kuwa ataendelea na morali hii.

"Nguvu yake nzuri uwanjani inatusukuma sisi sote kuendelea kupambana zaidi," aliongeza kusema Reus.

Haaland amekuwa mchezaji wa kwanza kufikisha magoli 10 katika timu moja ndani ya muda mfupi katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Amefunga mabao hayo 10 katika mechi saba alizoichezea Borussia Dortmund msimu huu.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SCHOLES AMTAJA DE GEA TATIZO UNITED

Nyota huyo wa zamani wa kikosi hicho amemtaka Solskjaer pia kuboresha nafasi ya beki wa kati...

**MANCHESTER, England**

PAUL Scholes amesema golikipa, David de Gea amekuwa ni tatizo halisi katika timu ya Manchester United na pia kunahitajika uboreshwaji wa nafasi ya beki wa kati.

Nyota huyo wa zamani wa United amesema anahitaji kuona kwenye usajili wa kocha Ole Gunnar Solskjaer wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja, kunafanyika maboresho makubwa.

Ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Newcastle kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, mwishoni mwa wiki, umewahakikishia vijana hao wa Old Trafford kuwa kwenye mbio na Manchester City katika kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

Walipata ushindi huo, lakini hawakuweza kuzuia nyavu zao kutikiswa kwa mara nyingine na maswali yamekuwa yakiulizwa juu ya kiwango cha timu, hasa safu yake ya ulinzi. Scholes ameiambia BT Sport madhaifu ya golikipa De Gea, kwamba hayupo imara langoni.

Kauli ya Scholes imekuja kutokana na De Gea, raia wa Hispania kufungwa bao ambalo lilikuwa kwenye uwezo wake wa kuokoa na mchezaji wa Newcastle, Allan Saint- Maximin baada ya mabeki kufanya uzembe.

"Tulilitaja hili kabla ya mchezo kuanza, nadhani huo ni upungufu mkubwa katika timu hii," alisema Scholes.

"De Gea tena, alifanya makosa baada ya kuzuia mpira wa kona iliyookolewa katika eneo baya.

"Kuna mambo De Gea anayafanya ambayo kwa akili ya kawaida unaona ni makosa ya kizembe ambayo yanaweza kurekebishwa, lakini hali inaendelea hivi katika kila mechi.

"Kwa namna yoyote usajili wa kipindi cha majira ya joto, Manchester United lazima ikubali kufanya maboresho kwenye nafasi ya golikipa, maana bila hivyo matatizo yatakuwa makubwa."

Pia Scholes akainyooshea kidole safu ya ulinzi ya United, kwamba nayo bado haijajipanga na inahitaji maboresho.

"Nafikiri beki ya kati kuna tatizo, kunahitaji maboresho ya haraka, inaonekana hakuna umakini mkubwa," alisema Scholes.

## KWA UFUPI

**MBAPPE, HAALAND KUMEKUCHA**

MGOMBEA urais wa Barcelona, Toni Freixa anaamini wataweza kuwasajili washambuliaji wa PSG na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, na nyota wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland (20). ***(Marca)***

**ISAK ANUKIA BARCA**

BARCELONA imeongeza nia yake ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 21. ***(ESPN)***

**HENDERSON NJIA MOJA**

GOLIKIPA wa England, Dean Henderson (23), atajaribu kuondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu, iwapo hatohakikishiwa kupata nafasi katika kikosi cha kwanza cha msimu ujao. ***(Manchester Evening News)***

**MOURINHO KUTI KAVU**

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikamwajiri Kocha wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann kuchukua nafasi ya Mreno Jose Mourinho. ***(Telegraph)***

**AGUERO AGOMBEWA ULAYA**

JUVENTUS na Inter Milan zimejiunga katika kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero (32), na raia wa Argentina, ambaye tayari amezungumza na Barcelona na Atletico Madrid kuhusu uwezekano kuhamia katika klabu hizo mwisho wa msimu huu. ***(Sun)***

**LINGARD AGEUKA LULU**

KLABU ya Manchester United imekataa kutoa baraka kifungu kitakachoruhusu West Ham kumsajili moja kwa moja, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 mwishoni mwa msimu huu. ***(Times)***

**DOHERTY NJIA PANDA**

MLINZI wa Ireland, Matt Doherty anakabiliwa na sitofahamu kuhusu hatima yake katika klabu ya Tottenham Hotspur, huku kocha Jose Mourinho akiondoa wasiwasi kuhusu mchezaji huyo. ***(ESPN)***

**SABITZER SOKONI**

RB Leipzig inajiandaa kumuuza mchezaji anayelengwa na Tottenham, Marcel Sabitzer ambaye ana umri wa miaka 26, huku wakitafuta mchezaji atakayechukua nafasi yake mwisho wa msimu huu. ***(Football Insider)***

**TUCHEL ALIMTAKA SUAREZ**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amekiri kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 34, wakati alipokuwa akiiongoza PSG, lakini kwa sasa hafikirii kumsajili nyota huyo wa zamani wa Liverpool pale Stamford Bridge. ***(London Evening Standard)***

**MARRISON SAFARI IMEIVA**

KLABU ya Huddersfield imethibitisha inafikiria kumsajili aliyekuwa kiungo wa kati wa West Ham, Ravel Morrison kwa uhamisho wa bure. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa sasa hana timu baada ya kuondoka ADO Den Haag ya Uholanzi hapo Januari mwaka huu. ***(Sun)***

**JAGIELKA AITAKA LIVERPOOL**

MLINZI wa kati wa Sheffield United, Phil Jagielka mwenye umri wa miaka 38, amesema yupo tayati kujiunga na Liverpool. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# AZAM FC YAENDELEA KUUKIMBIA UBINGWA

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kutoka sare ya bila kufungana na Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa juzi usiku, Kocha Msaidizi wa Azam FC Mrundi, Vivier Bahati, amesema wachezaji wake waliingia kwenye 'mtego' wa kuiga mfumo uliokuwa unatumiwa na wapinzani wao.

Matokeo hayo yaliifanya Azam FC ifikishe pointi 37 baada ya kucheza mechi 21 huku Tanzania Prisons iliyopo katika nafasi ya nane ilifikisha pointi 26 baada ya kushuka dimbani mara 20.

Yanga yenye pointi 49 inaendelea kuongoza katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 18 ikifuatiwa na mabingwa watetezi Simba wenye pointi 42, lakini wamecheza mechi pungufu tatu.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo kumalizika, Vivier alisema wachezaji wa Prisons walicheza mfumo wa kutumia nguvu na kugongana, kitu ambacho kilisababisha nyota wa timu yake kuiga aina hiyo ya mchezo na kuifanya mechi hiyo kuwa ngumu.

"Mchezo ulikuwa wa nguvu na kugongana. Tulitengeneza nafasi nyingi, hasa kipindi cha kwanza, lakini hatukuzitumia. Kipindi cha pili tuliongeza washambuliaji, tukawa tunacheza na mastraika wawili, lakini kwa sababu mipira yenyewe ilikuwa ya juu. Tulijiingiza wenyewe kwenye mtego, kwani tulikuwa tunapiga mipira ya juu kwa washambuliaji wetu, kumbe na wao wako vizuri kwa mipira ya aina hiyo," alisema Vivier.

Kocha huyo alisema endapo mawinga wake wangefungua na kupata nafasi ya kupiga krosi, hali ingekuwa tofauti, lakini hilo halikuwezekana kutokana na tayari wachezaji wao walikuwa wakiiga mchezo wa wapinzani wao. "Hatukuwa na bahati ya kupata pointi tatu kwa sababu mchezo ulikuwa wa kutumia nguvu kubwa, pia tulikosea kuwaiga walivyocheza wapinzani wetu, tumeliona kosa na hatutarudia katika mechi nyingine," Vivier alisema.

Aliongeza kikosi chake kilikuwa na wakati mgumu zaidi kwenye dakika 45 za kwanza, lakini kipindi cha pili walifanya mabadiliko na kuongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji ambayo haikuzaa matunda kwa sababu wapinzani wao walifanikiwa kuicheza mipira ya juu na kuondoa hatari.

"Haikuwa bahati kwetu, tulifanikiwa kutengeneza nafasi nyingi, lakini ilikuwa ngumu kuzitumia kwa kuwa muda mwingi wapinzani wetu wanafika katika eneo la tukio na kutupokonya mipira ya juu," alisema Vivier.

Baada ya mechi hiyo, Azam inajipanga kuwakaribisha Mbuni FC katika mechi ya mzunguko wanne wa mashindano ya Kombe la FA wakati Tanzania Prisons yenyewe itawafuata Sahare All Stars ya jijini Tanga kwenye hatua hiyo.



Kiungo wa kimataifa wa Simba Queens kutoka Burundi, Joelle Bukuru (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Ruvuma Queens, Eva Jackson katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena jijini Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Mwadui waomba msaada kujinasua

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Amri Said amesema ana kazi kubwa na anahitaji sapoti kubwa kutoka kwa uongozi wa timu hiyo ili kuhakikisha wanabakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao.

Mwadui FC inaburuza mkia ikiwa na pointi 15 baada ya kucheza mechi 21, huku timu nyingine zilizo kwenye hatari ya kushuka daraja ni pamoja na Mbeya City yenye pointi 15, Ihefu FC yenye pointi 20 sawa na Gwambina FC ya jijini Mwanza.

Amri aliliambia gazeti hili ili kuondoka katika hatari hiyo, mabosi wake wanatakiwa kuongeza nguvu na ushirikiano kwenye timu kwa sababu uwezo wa kupambana kufanikisha wanatimiza malengo ya kubaki kwenye ligi hiyo wanao.

Beki huyo wa zamani wa Simba alisema wachezaji wake wataendelea kupambana kutafuta matokeo chanya katika michezo iliyopo mbele yao lakini hilo litawezekana endapo mahitaji muhimu yatatekelezwa.

"Tumepoteza pointi sita, sio kama tumecheza vibaya hapana, ukiangalia mechi yetu dhidi ya KMC FC, tumecheza vizuri lakini kuna makosa madogo ambayo wapinzani wetu waliyatumia na kutufunga, kuna mabadiliko katika kikosi changu kwa kutazama kiwango kilichoonyeshwa tulipocheza dhidi ya Biashara United na KMC FC," alisema Amri.

Aliongeza upungufu ambao bado unaitesa timu yake kwenye safu ya ulinzi ambayo inakosa umakini na utulivu na hivyo kuruhusu mashambulizi ya mara kwa mara katika lango lao.

## Waogeleaji 150 kuchuana Taliss

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU sita zimethibitisha kushiriki katika mashindano ya kuogelea ya Taliss yaliyopangwa kufanyika Jumamosi na Jumapili kwenye bwawa la kuogelea la klabu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Meneja wa klabu ya Taliss, Hadija Shebe alizitaja klabu hizo ni ya Dar es Salaam (DSC), Bluefins, Mwanza, FK Blue Marlins, Mis Piranhas na wenyeji Taliss.

Shebe alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika na klabu hizo zitakazochuana zinaendelea kujiimarisha ili kuwania medali na vikombe mbalimbali vitakavyotolewa.

Aliwataja wadhamini wa mashindano hayo kwa mwaka huu ni pamoja na benki ya NMB, Smiles Car, Jubilee Insurance, Azam, Pepsi, Klabu ya Gymkhana, ITV Media, Knight Support, Kampuni ya Champion Rise, Flames, The Range, Justfit Sports Gear, Tarmal Industries na A2 Washpoint.

"Tunatarajia kuwa na waogeleaji zaidi ya 150 kushiriki. Pia tunatarajia kuona ushindani mkubwa katika mashindano haya ya kwanza kufanyika tangu serikali iliruhusu michezo kurejea tangu Juni, mwaka jana," alisema meneja huyo.

Aliongeza ili kuleta ushindani wa kweli, kila mwogeleaji atashindana katika matukio nane, sita ya mmoja mmoja na mawili ya kundi maarufu kwa jina la 'relay'.

Alisema siku ya kwanza, waogeleaji watashindana katika matukio 71 na siku ya pili kutakuwa na matukio 34.

## Washindi Betika Deile wazawadiwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubahatisha ya Betika imewatangaza washindi watatu wa Jackpot yake ya 'Kitonga Deile' inayofanyika kila siku ambao wamejinyakulia kitita cha Sh. milioni 21.3.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Utawala na Fedha wa kampuni hiyo, Deodata Kalumia alimtaja mshindi wa kwanza kuwa ni Habib Juma ambaye ni dereva wa bodaboda wa Arusha ambaye amejinyakulia Sh. milioni 13.4.


Kalumia alisema mshindi huyo alibashiri kwa usahihi kwa kutumia dau la Sh. 1,000.

Alisema ushindi wa Juma unatoa fursa ya ajira kwa vijana kama akiamua kununua bodaboda nyingine kwa kutumia fedha hizo za zawadi alizopokea kupitia shindano hili.

"Juma sasa yuko katika nafasi nyingine tofauti, kupitia zawadi aliyopata anauwezo wa kununua bodaboda sita ambazo zitamwezesha kuongeza kipato chake," alisema Kalumia.

Alimtaja mshindi wa pili katika jackpot hiyo ni Shaban Hayuma kutoka Dodoma ambaye amejinyakulia Sh. milioni 4.4 baada ya kuweka dau la Sh. 2,000 huku mshindi wa tatu akiwa ni mfanyabiashara, Mohamed Nassor aliyeshinda Sh. milioni 3.3 baada ya kuweka dau la Sh. 1,000.

Michezo
Jumatano Februari 24, 2021
Nipashe



SCHOLES AMTAJA DE GEA TATIZO UNITED

HABARI UK 22




Winga wa Simba, Luis Miquissone (katikati), akijiandaa kupiga shuti huku golikipa wa Al Ahly, Ahmed El Shenawy (kushoto) akifanikiwa kuondoa hatari kwenye lango lake katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YANGA YAIANDALIA 'MAUAJI' KENGOLD

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kikosi chake kitaingia tofauti katika mechi ya mzunguko wa nne wa mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Kengold ili kujihakikishia ushindi mnono na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Kaze alisema anataka kuona kikosi chake kinapata mabao mengi katika mechi hiyo ili kuongeza morali kabla ya kurejea kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo iko kwenye mzunguko wa pili.

Kocha huyo alisema amewataka wachezaji wake kuongeza utulivu na kuzitumia vyema nafasi za kufunga wanazozitengeneza na kwa kufanya hivyo, watafikia mapema malengo yao.

"Tunajua mechi hiyo ni sawa na fainali, kwa sababu ili uendelee na mashindano ni lazima ushinde, tunataka kuwapa furaha mashabiki wetu, tumejipanga na tunaendelea kujiimarisha kuelekea mechi hiyo muhimu," Kaze alisema.

Kocha huyo alisema wachezaji wake waliokuwa majeruhi akiwamo kiungo Mkongomani Mukoko Tonombe ambaye aliumia katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar hali yake imeimarika na yuko tayari kuitumikia Yanga katika mechi inayofuata.

Yanga itaikaribisha Kengold FC Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Simba wao watawavaa African Lyon siku inayofuata.

# SIMBA BABA LAO

## ●●●Yaichapa Al Ahly 1-0 na kuongoza katika Kundi A...

**Na Adam Fungamwango**

SIMBA baba lao. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya mabingwa hao wa Tanzania mara tatu mfululizo sasa, kuwafunga mabingwa wa Afrika, Al Ahly kutoka Misri bao 1-0.

Katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, raia wa Msumbiji, Luis Miquissone, maarufu kama Konde Boy, ndiye aliyefunga bao hilo pekee ambalo limeiwezesha Simba kufikisha pointi sita na kukaa kileleni mwa Kundi A la michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Miquissone alifunga bao hilo dakika ya 31 baada ya kuupata mpira nje ya eneo la hatari, akawazungusha mabeki wa Al Ahly na kuachia shuti kali la mguu wa kushoto kisha mpira kugonga mwamba wa juu, ukatinga wavuni.

Kwa ushindi huo, Simba imeendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi yoyote kwenye ardhi ya Tanzania, ikicheza na timu za Afrika Kaskazini, maarufu kama Waarabu kwenye historia ya klabu hiyo.

Kama vile haitoshi, inakuwa mara ya tatu kuifunga Al Ahly nchini Tanzania. Mara ya kwanza ikiwa mwaka 1985 ikishinda mabao 2-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza na mara ya pili Februari 12, 2019 ikishinda bao 1-0 kwenye michuano kama hii hatua ya makundi, zilipokuwa kwenye Kundi D.

Lakini inaendeleza rekodi yake safi ya kutopeteza mechi yoyote ya kimataifa kwa miaka saba sasa ikicheza nchini Tanzania. Mara ya mwisho ilifungwa kwenye Kombe la Shirikisho la Afrika, Februari 17, 2013 dhidi ya Recreativo do Libolo ya Angola.

Katika mechi ya jana, kila timu ilionyesha uwezo wa hali ya juu, huku zikishambuliana kwa zamu, lakini Simba ikikosa mabao mengi.

Dakika ya sita tu, Luis Miquissone nusura aipatie Simba bao, kama si kuukokota sana mpira na kusukumwa kidogo na beki wa Al Ahly kabla ya kuanguka na mpira kuwahiwa na kipa Ahmed Al Shenawy.

Shomari Kapombe alichelewa kuuwahi mpira uliotangulizwa mbele yake, akiwa kwenye eneo la hatari na kipa Shenawy akauwahi.

Dakika ya 16, Kahraba aliwahadaa mabeki wa Simba, Joash Onyango na Paschal Wawa, akaachia shuti kali lililopita juu ya lango la Simba. Wachezaji wa Simba walipata kigugumizi cha kuuweka mpira wavuni, uliopigwa na Miquissone ukizua kizaazaa kwenye lango la Al Ahly, kabla ya mabeki wa timu hiyo kuufagia na kuondosha hatari.

Dakika moja baadaye, Walter Bwalya aliruka juu na kuupiga kichwa mpira uliotoka nje kidogo ya lango la Simba. Kipa El Shenawy, aliwaokoa Al Ahly dakika ya 39, alipopangua shuti la Chriss Mugalu na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa Thadeo Lwanga aliyeumia na kuingia Erasto Nyoni, Meddie Kagere akichukua nafasi ya Mugalu, na Francis Kahata nafasi ya Miquissone, Clatous Chama akitoka na ikachukuliwa na Kennedy Juma.

Mzamiru Yassin aliikosesha Simba bao dakika ya 71 baada ya shuti lake kuzuiwa na beki, Yasser Ibrahim na kuwa kona.

Dakika tano za mwisho, Al Ahly ilicharuka na kukosa mabao mawili ambayo yangeleta majonzi kwa Watanzania. Dakika ya 85, Mohamed Wahid aliikosesha timu yake bao, alipopiga mpira ulitoka nje ya lango.

Aishi Manula aligeuka kuwa shujaa dakika moja kabla mechi kumalizika, alipopangua kwa ustadi shuti la Mahmoud Kahraba.

Aidha, katika mechi nyingine ya kundi hilo iliyochezwa jana, AS Vita ikiwa ugenini jijini Khartoum nchini Sudan ilipata ushindi wa mabao 4-1, dhidi ya wenyeji El Merrik.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002